

Mtumiaji

Jarida la habari zenyet kuwajengea uelewa watumiaji wa huduma za Nishati na Maji

ISSN 2738-9014

Toleo Na. 11 • Januari - Juni, 2025



HALIUZWI

Mhe. Kapinga
aipongeza
EWURA CCC
kwa elimu,
nishati safi

Baraza
laimarisha
uwakilishi,
utetezi
watumiaji

71.2%

Asilimia ya
malalamiko 2,368
yaliyoshughulikiwa
kikamilifu

Nishati Safi ya Kupikia ndiyo mpango mzima



Kutoka Ofisi ya Katibu Mtendaji

Karibu kwenye toleo la 11 la Jarida la Mtumiaji, ambalo ni Jarida maalum linaloandalishi na kuchapishwa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, zinazodhibitiwa na EWURA. Jarida hili linalegenga kukuza uelewa na kushirikisha watumiaji wa huduma za nishati na maji nchini, kuhusu masuala yanayohusu huduma hizo.

Toleo hili limesheheni maarifa muhimu kuhusu masuala ya msingi ambayo mtumiaji wa huduma za nishati anapaswa kujifunza na kuyaelewa ili kuwa na matumizi yenye tija katika ngazi ya kaya na taifa kwa ujumla. Pamoja na mambo mengine, kupitia Jarida hili, msomaji utapata fursa ya kuzifahamu haki na wajibu wako.

Aidha utapata kuelewa jithada zinazofanywa na Baraza katika kuelimisha watumiaji kuhusu matumizi ya sahihi ya nishati safi ya kupikia, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono na kuendeleza ajenda ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, inayolenga kufanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2034. Tunaamini kuwa maarifa haya na mengine mengi yaliyomo kwenye Jarida hili yatasaidia kujenga jamii yenye uelewa mpa na kuhusu masuala ya huduma zinazodhibitiwa na EWURA.

Ukiwa Mtumiaji wa huduma za nishati na maji, wewe ni mdau muhimu katika maendeleo endelevu ya sekta hizi. Ni dhamira ya Baraza kuhakikisha kuwa, unapokea elimu ya kutosha kuhusu nafasi yako katika kuboresha huduma za nishati na maji unazotumia.

Tunakuhamasisha kutenga muda wako ili ujelimishe kuhusu masuala yanayokuhusu kupitia toleo hili, ambalo Habari, Makala, na taarifa zingine zimewasilishwa kwa mtiririko maalumu ili kurahisisha usomaji na ufuutiliaji wa taarifa zilizomo.

Asante kwa kuwa sehemu ya wasomaji wetu waaminifu. Tunakutakia usomaji mwema na wenye manufaa!



Stella Lupimo
KATIBU MTENDAJI



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga akipata maelezo toka kwa Afisa Huduma kwa Wateja EWURA CCC Mbeya Bi Mwasiti Majengo, alipotembelea banda la EWURA CCC wakati wa tamasha la *Tulia Cooking Festival* liliofanyika Agosti 2024, katika viwanja vya Rwanda Nzovwe jijini Mbeya.

Mhe. Kapinga aipongeza EWURA CCC kwa elimu ya nishati safi

Na Mwasiti A. Majengo, Mbeya

Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga amelipongeza Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kwa ushiriki wake kwenye maadhimisho ya tamasha la "Tulia Cooking Festival 2024," na kutoa elimu kuhusu huduma za nishati safi ya kupikia ambapo kilele chake kili-fanyika tarehe 31 Agosti 2024 jijini Mbeya.

Mhe. Kapinga ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la EWURA CCC kwenye kilele cha maadhimisho hayo, ambapo ye ye ndiye alikuwa mgeni rasmi.

"Nimefurahi kuwaona EWURA CCC katika tamasha hili, na ni nawapongeza kwa kazi kubwa mnay-ofanya ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu faida za kutumia nishati safi

ya kupikia. Hii ni hatua kubwa na muhimu kwa taifa katika kuhakikisha wananchi wanapata uelewa wa matumizi sahihi ya nishati hii, ambayo ni salama na rafiki kwa mazin-gira," alieleza Mhe. Kapinga.

Katika tamasha hilo Baraza lille-toa elimu kwa wadau mbalimbali walio tembelea banda lake, ikiwemo kuhamasisha matumizi salama ya nishati safi ya kupikia, athari zin-azoweza kusababishwa na matumizi yasiyo sahihi, elimu kuhusu afya ya watumiaji pamoja na usalama wa mali zao wanapotumia nishati hiyo.

Elimu hiyo pia ilitolewa kupitia majukwaa ya matangazo, kufanya mahojiano na vyombo mbalimbali vya habari pamoja na kusambaza vi-peperushi kwa watu waliohuduria tamasha hilo.

Eneo jingine liliofundishwa kupitia hadhira hiyo na hadhira mbalimbali ni pamoja na umuhimu wa kupi-

ma uzito wa mitungi ya gesi wakati wa kununua ili kuhakikisha ujazo sahihi ukilinganisha na uzito ulioandikwa kwenye mtungi ili kuhakikisha mtumiaji anapata bidhaa inayolingana na thamani halisi ya fedha anazolipia.

Akitoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya nishati kwa makundi mbalimbali ya watumiaji, ndugu Lusekelo Kajela, Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji mkoani Mbeya, alisisitiza watumiaji wa gesi kujenga tabia ya kusafirisha mitungi ya gesi iki-wa wima, kuihifadhi sehemu yenye hewa ya kutosha na mbali na vyanzo vya moto ikiwa ni njia salama ili kue-pushu hatari ya mtungi kulipuka.

Tamasha la *Tulia Cooking Festival* 2024, liliofanyika kwa kushirikisha Kampuni ya gesi ya ORXY kuanzia Agosti 27 na kumalizika Agosti 31, 2024 likiwa limebeba kaulimbiu ya "Nishati Safi Kwa Wote."

Baraza laimarisha uwakilishi, utetezi watumiaji

Na Lugiko I. Lugiko, Dodoma

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2024. Mafanikio haya yametokana na mi-pango madhubuti na ushirikiano wa karibu na wadau mbalimbali, hatua ambayo imelifanya Baraza kuwa nguzo muhimu katika kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji nchini zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Akizungumza na mwandishi wa habari hii hivi karibuni, katika ofisi za

Baraza zilizoko jijini Dodoma, Katibu Mtendaji wa EWURA CCC, Bi. Stella Lupimo, alielea kwamba kazi kubwa iliyofanywa na Baraza imejikita katika kuimarisha uelewa wa watumiaji kuhusu haki na wajibu wao, kuwakilishi watumiaji katika uandaaji wa miongozo mbalimbali katika sekta za nishati na maji, pamoja na kushughulikia malalamiko yaliyopokelewa kutoka kwa watumiaji.

Kwa mujibu wa ripoti za utendaji wa Baraza, kipindi cha Julai hadi Desemba 2024 kimeshuhudia utekelezaji wa jumla ya programu 703 za uelimishaji wa umma. Kupitia programu hizi, Baraza limefanikiwa kuwafikia jumla ya watu 134,273 kutoka makundi mbalimbali ya jamii, ikiwa ni

juhudu za kuhakikisha wananchi wanapata maarifa sahihi kuhusu huduma wanazopokea.

Makundi yaliyofikiwa katika programu hizi ni pamoja na waumini katika makanisa na misikiti, wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, vyuo pamoja na walimu na wakufunzi wao, makundi ya vijana, makundi ya akina mama, madereva wa bodaboda, maafisa wa Jeshi la Magereza na Jeshi la Zimamoto, pamoja na wananchi kwa ujumla kupitia mikutano ya serikali za mitaa.


Bi. Lupimo alisema, "Tumefanya juhudu kubwa kuhakikisha elimu inawafikia walengwa, kwani tunaamini uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya nishati na maji ni muhimu katika kuboresha huduma hizi. Watumiaji wanapokuwa na ufahamu, wanakuwa na uwezo wa kudai haki zao na kushirikiana na watoa huduma katika kutatua changamoto zinazojitekeza."

Kwa upande wa utatuvi wa malalamiko, Baraza limepokea jumla ya malalamiko 2,368 katika kipindi hicho. Kati ya malalamiko hayo, 832

Inaendelea Uk. 6



Katibu Mtendaji wa Baraza Bi. Stella Lupimo akimweleza Profesa Anna Tibaijuka namna Baraza linavyotekeleza majukumu yake na kuwafikia watumiaji alipotembelea banda la EWURA CCC wakati wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Julai 2024.



Tupambane kikamilifu na mabadiliko ya tabianchi

Mabadiliko ya tabianchi ni changamoto kubwa inayolikabilii taifa letu, Tanzania. Athari zake zimeonekana wazi kupitia ukame unaopunguza upatikanaji wa maji, mafuriko yanayoharibu miundombinu na mabadiliko ya mifumo ya mvua yanayoathiri uzalishaji wa umeme na mazao ya chakula na biashara.

Sekta za nishati na maji ni nguzo muhimu za maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hivyo upo wajibu mkubwa katika kukabiliana na changamoto hizi. Baraza, linawajibika kuhakikisha kuwa maslahi ya watumiaji yanalindwa katika juhudzi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, Tanzania imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya nishati mbadala kama vile sua, upepo na maji. Serikali, kupitia Mkaatini wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034), inalenga kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia kufikia asilimia 80 ya Watanzania ifikapo mwaka 2034.

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) ikiwa ni mionganoni mwa wadau wakubwa wa utekelezaji wa Mkakati huu, tunahimiza utekelezaji wake kwa kuhamasisha sera na uwekezaji unaochochaea matumizi ya nishati mbadala ambayo ni rafiki kwa mazingira na nafuu kwa watumiaji wa kipato cha chini.

Katika sekta ya maji, mabadiliko ya tabianchi yameathiri upatikanaji wa maji safi na salama. Kupungua kwa vyanzo vya maji na ukame vimeongeza changamoto kwa watoa huduma na watumiaji. Ripoti ya 15 ya EWURA ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na

Usafi wa Mazingira nchini, iliyozinduliwa Machi 2024 na Wizara ya Maji, inaonesha umuhimu wa kuboresha huduma za maji ili kukabiliana na changamoto hizi.

Baraza tunahimiza uwekezaji katika teknolojia za kisasa za kuhifadhi maji, kuboresha usambazaji na kupunguza upotevu wa maji. Pia, tunasisitiza watumiaji wa makundi yote kuwa na matumizi endelevu ya maji hasa katika kilimo na viwanda ili kuhakikisha upatikanaji endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Elimu kwa watumiaji ni sehemu muhimu ya juhudi zetu. Tunawahimiza watumiaji kuelewa jinsi wanavyoweza kuchangia kupambana na mabadiliko ya tabianchi kwa kubadili tabia zao, kama vile kutunza vyanzo vya maji, kupunguza matumizi ya siyo ya lazima ya nishati na maji na kuunga mkono huduma zinazozingatia ulinzi wa mazingira. Tunajivunia kuwa kiungo kati ya watoa huduma na watumiaji, tukihakikisha kuwa taarifa muhimu zinawafikia wananchi kwa uwazi, weledi na kwa wakati.

EWURA CCC inaanini kuwa kupambana na mabadiliko ya tabianchi ni jukumu la kila mmoja wetu. Kwa kushirikiana na Serikali, watoa huduma na watumiaji, tunaweza kuboresha sekta za nishati na maji ili kuwa endelevu zaidi. Hii itahakikisha sio tu kuwa tunakabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, bali pia tunaboresha maisha ya Watanzania kwa ujumla.

Ni wakati wa kuchukua hatua sasa, kwa maslahi ya taifa letu na vizazi vijavyo. EWURA CCC iko tayari kuendelea kuwateeta na kuwalinda watumiaji wa huduma hizi muhimu.

BODI YA UHARIRI
Ms. Stella Lupimo
- Mwenyekiti na Mhariri Mkuu
Geofrey Sokesia - Mhariri Msanifu
Lugiko L. Lugiko - Mjumbe
Chipegwa Samwel - Mjumbe
Anadoris Komba Mjumbe
Emmanuel Chagu Paul - Mjumbe

Wachangiaji
Amani Mbogo
Anadoris Komba
Brenda Magoma
Catherine Charles Ochido
Chipegwa Samwel
Emmanuel Paul
Geofrey Sokesia
Lugiko Lugiko
Magreth Temba
Mwasiti Athuman
Neema Nnko
Noela Ntiluvakule
Nuru Zuberi
Ramadhan Kakende
Said Ismail
Sakina Yusuf
Theresia Mande
Wadi Omari
Zamda Mabada

Mawasiliano
Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la PSSSF, Mtaa wa Kambarage,
Barabara ya Jakaya Kikwete,
S.L.P. 772, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 026 296 0099
Simu: +255 746 482 008
Baruaapepe: info@ewuracc.go.tz
Tovuti: www.ewuracc.go.tz

Inatoka Uk. 4

Baraza laimarisha uwakilishi, utetezi

yalihusu huduma za maji, 1,441 yalihsu huduma za umeme, 35 yalihusu huduma za gesi ya kupikia majumbani (LPG) na 60 yalihusu huduma nyinginezo.

Bi. Lupimo alibainisha kuwa kati ya malalamiko hayo, 1,685 sawa na asilimia 71.2 ya malalamiko yote yameshughulikiwa kikamilifu. Malalamiko yaliyosalia, ambayo ni 683, sawa na asilimia 28.8 bado yako kwa watoa huduma kwa hatua za utatuza.

Bi. Lupimo alibainisha kuwa, "Ushirikiano wetu na watoa huduma umekuwa wa manufaa makubwa katika kuhakikisha changamoto za watumiaji zinatatuliwa kwa haraka na kwa ufanisi."

Alieleza katika hatua nyingine kuwa, Baraza lilishiriki kufanya mapitio ya Rasimu ya Kanuni za Umeme za Mwaka 2024 pamoja na ya Rasimu ya Mwongozo wa Mpango wa Usafi wa Mazingira kwa mamlaka za maji, zote zikiwa zimeandalialiwa na EWURA. Katika hatua hii, Baraza liliwasilisha maoni yake kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, yaani EWURA.

miongozo hiyo."

Aidha, Bi. Lupimo alisisitiza kuwa mafanikio haya hayangewezekekana bila mipango madhubuti ya Baraza, usimamizi bora, na ushirikiano na wadau mbalimbali. Wadau hao ni pamoja na Wizara ya Nishati, EWURA, watoa huduma za nishati na maji, taasisi za Serikali na viongozi wa Serikali za Mitaa, pamoja na makundi mbalimbali katika jamii.

"Mafanikio haya ni ushahidi wa kazi kubwa inayofanywa na Baraza, lakini pia ni matokeo ya ushirikiano wa karibu na wadau wetu. Tutaendelea kuimarisha juhudhi hizi ili kuhakikisha maslahi ya watumiaji yanalindwa na changamoto zinazojitokeza zinatatuliwa kwa wakati," aliongeza Katibu Mtendaji.

Ripoti za EWURA CCC zinaonesha kwamba Baraza limeendelea kuwa chombo muhimu na cha kuanminika kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji nichini, na limeonesha dhamira thabiti ya kutekeleza majukumu yake kwa manufaa ya wananchi.

Baraza litaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi kadri itakavyowezekana kwa kushirikiana na wadau wote ili kuharakisha utoaji wa elimu kwa watumiaji ambaa hawajafikiwa.

Mafanikio haya ni ushahidi wa kazi kubwa inayofanywa na Baraza, lakini pia ni matokeo ya ushirikiano wa karibu na wadau wetu. Tutaendelea kuimarisha juhudhi hizi ili kuhakikisha maslahi ya watumiaji yanalindwa na changamoto zinazojitokeza zinatatuliwa kwa wakati

Katibu Mtendaji huyo alinukuliwa akieleza umuhimu wa Baraza kushiriki katika mapitio ya miongozo akisema, "Ushiriki wa Baraza katika michakato hii ni muhimu ili kuhakikisha kwamba maoni na maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji yanazingatiwa katika mchakato wa uundaji wa kanuni au



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (TUWASA)



IJUE TUWASA



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (**TUWASA**)
 Inadhamana ya Kuzalisha na Kusambaza Majisafi na Kusimamia
 Huduma za Usafi wa Mazingira katika **Manispaa ya Tabora, Isikizya, Sikonge, Urambo na Kaliua**

0800780063 tuwasatabora.tz @tuwasa_tabora www.tuwasa.go.tz



Toeni elimu zaidi kwa watumiaji - Kamishna Jeshi la Zimamoto

Na Catherine Charles, Ilala

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkao wa Ilala, imeshauriwa kuongeza jitihadi katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ili kuongeza uelewa kwa watumiaji na kuweza kutambua haki na wajibu wao.

Wito huu ultolewa hivi karibuni na Kamishna Msaidizi Mwandalamizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Bw. Peter Mabusi, ofisini kwake Upanga jijini Dar es Salaam alipotembelewa na Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkao wa Ilala, kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.

Akifundisha kuhusu kazi za Baraza, Bi. Mary Nyato, Katibu wa Kamati hiyo alieleza kuwa, moja ya majukumu ya Baraza ni kuwawakilisha watumiaji wa huduma za nishati na maji katika vyombo vya maamuzi ikwemo Wizara ya Nishati na EWURA.

Elimu nyiningine iliyotolewa ni kuhusu matumizi sahihi na endelevu ya huduma, haki na wajibu wa watumiaji wa huduma hizo zikiwemo haki ya

kupata huduma ilio salama, kufidiwa kutokana na hasara au bidhaa zenye dosari na kupatiwa taarifa muhimu zinazohusu huduma hizo.

"Kila mtumiaji ana haki ya kupata huduma ilio bora na salama, kuelimishwa kuhusu huduma anayopata, haki ya kuwa katika mazingira bora, haki ya kufidiwa na haki ya kusikilizwa na kuwalishwa," alisema Bi. Nyato.

Pamoja na elimu hiyo, Kamishna Mabusi, aliiomba Kamati hiyo kuzidi kutembelea makundi mbalimbali ya watumiaji na kuwaelimisha, ili waweze kunufaika na elimu hiyo muhimu inayogusa moja kwa moja maisha yao ya kila siku.

"Elimu mnayofundisha ni ya muhimu sana kwa jamii. Kwa mfano, suala la matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji ni muhimu sana ambayo watumiaji wengi wanapaswa waipate. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, jamii kubwa ya Watazania ina uelewa mdogo wa elimu hii, hali inayopelekea uharibifu wa miundombinu, kupata bili kubwa za maji, madhara ya kiafya, majanga ya moto na hata vifo pindi huduma hizi zitapotumika vibaya," alisema Kamishna Mabusi.

Alieleza kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaamini kuwa elimu, hasa

Bi. Mary Nyato, Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkao wa Ilala, akitabidhi nakala ya Jarida la Mtumiaji kwa wanajeshi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kituo cha Upanga, jijini Dar es Salaam, baada ya kutoa elimu kuhusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.

Picha na Catherine Charles

kuhusu mambo ya umeme, gesi na mafuta, itasaidia kupunguza maafa ya moto katika jamii.

Naye Katibu wa Kamati ya Watumiaji Mkao wa Ilala Bi. Mary Nyato alimshukuru Kamishna Mabusi kwa kuwapatia nafasi kuwaelimisha watumishi wa Jeshi la Zimamoto.

Bi. Nyato alisema "Kamati yetu imejipanga kutekeleza programu mbalimbali ambazo lengo lake ni kufikia makundi mbalimbali ya watumiaji na kuwapatia elimu hii muhimu ili waweze kutambua haki zao za msingi na kuzingatia wajibu walio nao kufanya huduma hizi ziwe endelevu."

Alisema Kamati ya Mkao wa Ilala ina utaratibu wa kufikia makundi mbalimbali ya watumiaji mahali walipo, kama vile shulen, hospitalini, masokoni, ofisini na sehemu ambazo zina mkusanyiko mkubwa wa watu, ikiwa ni mkakati wa kufikia watumiaji wengi zaidi.

Bi. Nyato alimuahidi Kamishna huyo kuwa Kamati yake itafanya kazi ushauri wake lakini alimwomba Kamishna huyo kuipatia fursa wakati mwingine Kamati hiyo kutoa elimu kwa wanajeshi wengi zaidi wa jeshi hilo.



Afisa Huduma kwa Wateja na Utawala EWURA CCC Dodoma Bw. Amani Mbogo, akitoa elimu juu ya Matumizi sahihi ya Huduma za Nishati na Maji kwa Jumuiya ya Kina Mama wa Kiislamu Tawheed Changombe mnamo tarehe 4/11/2024.

EWURA CCC yaunga mkono ajenda nishati safi ya kupikia

Na Mwandishi wetu, Dodoma

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Dodoma, imeunga mkono kwa vitemdo ajenda ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanza kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa makundi mbalimbali ya akina mama mkoani hapa.

Akitoa elimu hii kwenye Jumuiya za akina Mama wa Kiislamu wa Kata za Chamwino na Changombe Jijini Dodoma hivi karibuni, Afisa Huduma kwa Wateja Mwandamizi wa EWURA CCC Nd. Amani Mbogo aliwaleza akina mama wa Jumuiya hizo kuwa, nishati safi ya kupikia majumbani kama vile umeme na gesi za kupikia majumbani, maarufu kama "Liquefied Petroleum Gasa (LPG)" ni rafiki na rahisi kupikia na vilevile ina faida kubwa kwa watumiaji endapo watautumia kwa usahihi.

Akitoa mfano wa matumizi ya LPG ndugu Mbogo alisema "moja ya faida ni kuwa mitungi hii inapatikana kwa

urahisi karibia maeneo yote ya jiji la Dodoma na maeneo mengine nchini. Kutumia gesi hii na aina nyininge ya nishati safi inakuepusha na madhara ya kiafya kwani moshi unaotokana na matumizi ya nishati isiyo safi kama vile kuni na mkaa huwa na gesi zenye sumu pamoja na chembe-chembe ndogo zenye viambata vya sumu ambavyo huweza kudhoofisha mfumo wa upumuaji na kusababisha magonjwa kama kikohoz, pumu na mengineyo."

Ndugu Mbogo aliongezea kuwa, kwa kutumia gesi katika mapishi akina mama wataepukana na maradhi yatokanayo na moshi na kuepusha athari kubwa za kimazingira zinazosabibishwa na matumizi ya kuni na mkaa.

"Tunawahimiza kuendelea kutumia nishati safi ya kupikia ili kuitunza afya na mazingira yetu ya mkoao kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo. Pia niwasili kuwashamasisha na wadau wengine kuanza kutumia nishati hii kwani ni rahisi kuitumia," alisema ndugu Mbogo.

Akiongea wakati wa programu hiyo ya uelimishaji, mmoja wa viongozi wa jumuiya hizo akina mama

Bi. Hamisa Ali aliishukuru EWURA CCC kwa elimu waliyoipata na kuhamisika kuanza kutumia nishati hiyo kwani inaokoa muda wakati wa kupika.

"Ni kweli kwamba nishati safi ya kupikia inarahisha kazi na kuo-ko muda wa mapishi hivyo akina mama tunaweza kuokoa muda wa kuwa jikoni na kuutumia katika shughuli zingine za uzalishaji kiu-chumi, hivyo tunaishukuru sana EWURA CCC kwa elimu hii," alisema Bi. Hamisa.

Aliomba Ofisi ya EWURA CCC Mkoa wa Dodoma kutokuishia kutoa elimu hiyo kwa akina mama hao tu bali ijitahidi kueneza kwa makundi mengine ya akina mama ikizingatiwa kuwa wahanga wakub-wa wa nishati chafu ni akina mama kwani wao mara nyingi ndio wan-ofanya shughuli za jikoni.

Naye Bi. Khadija Hamisi kutoka Jumuiya ya akina Mama Tawheed Changombe, alieleza namna alivy-ofaidika na elimu hiyo lakini pia alionomba EWURA CCC kupanua wigo katika utoaji wa elimu hiyo ili iweze kutolewa kwa makundi yote ya Jumuiya za akina mama jijini Dodoma.

"Kabla sijapata elimu hii niliamini kuwa matumizi ya gesi ni anasa lakini pia niliamini kuwa wanaowenza kutumia gesi za kupikia ni lazima wawe watu wenyewe kipato cha juu sana. Kulikuwa na dhana kwamba mitungi ya gesi ni hatari na inaweza kulipuka muda wowote na kusababisha nyumba kuungua. Hali hii ilinifanya niogope kuijingiza kwenye matumizi ya gesi za kupikia, hata hivyo leo baada ya kupata elimu kutoka EWURA CCC juu ya faida ya matumizi sahihi na salama nime-hamasika kiasi kwamba nitaenda kumshauri mume wangu tununue mtungi wa gesi," alisema Bi. Khadija.

Ndugu Mbogo alihitimisha kwa kwa kumshukuru Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Mustapha Shabani kwa kutoa kibali kwa EWURA CCC kufanya program za uelimishaji kwa waumini wa Kiislamu Mkoa wa Dodoma, huku akione-sha utayari wa kuelimisha makundi mengine ya waumini pindi nafasi itakapopatikana.

VICOBA Ruvuma washauriwa kudai haki zao

Na Magreth Temba, Ruvuma

Wanachama wa vikundi mbalimbali nya VICOBA mkoani Ruvuma, wameshauriwa kuto-kaa kimya na kunung'unika wanapokuwa hawajardishwa na utoaji wa huduma za nishati na maji katika maeneo wanayoishi.

Ushauri huo umetolewa hivi karibuni na Mjumbe wa Kamati ya watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Ruvuma Bw. Ladislau- si Bigambo, alipokuwa akitoa elimu kwa wanachama wa vikundi nya VI- COBA kuhusu hatua za kuwasilisha malalamiko yanayohusu huduma za nishati na maji.

"Ukiona watoa huduma hawaja-kutende haki na huduma unaipata tofauti na matarajio yako, basi usi- shie tu kulalamika kwa wenzako mtaani kwani hautapata msaada sa-

hihi, badala yake peleka malalamiko yako kwa mto huduma husika au fika Ofisi za EWURA CCC Mkoa wa Ruvuma kwa msaada zaidi," alisema Bw. Bigambo.

Aliwasihii wanachama hao ku-hakikisha wanaitumia vyema elimu walioipata na kuwaelimisha wananchi wengine ambao wamekosa elimu hiyo muhimu.

Aidha aliwaelimisha wanakundi hao kuhusu vidokezo muhimu kama vile matumizi sahihi ya maji na nishati ili huduma hizo zisigeuke kuwa kero kwao.

"Hakikisha unafunga bomba la maji kila unapomaliza kutumia na usiache bomba wazi kama maji haya-toki kwani maji yakianza kutoka bila wewe kuwepo yanaweza kumwagi-ka na kukusababishia bili kubwa," alieleza Bigambo.

Kuhusu umeme, aliwaelimisha umuhimu wa kuzima taa kila panap-

opambazuka au kuwa na taa zinazo-jiwasha na kujizima kulingana na hali ya mwanga, kwani kwa kufanya hivo kunapunguza gharama za umeme zisizo za lazima pale umeme unapokuwa unawaka bila matumizi.

Naye Bw. Charles Msilu, Mwenyekiti wa Umoja Kikoba cha Umoja SILC alilishukuru Baraza mkoani humo kwa kufika katika Kikoba chao na kutoa elimu hiyo muhimu kwa wanachama kwani inagusa mojamoa maisha yao ya kila siku na hivyo imewafikia kwa wakati muafaka.

"Leo tumapata elimu mpya na muhimu sana katika matumizi ya umeme na maji. Nipende kuishuku-ru EWURA CCC kwa kufika katika vi-kundi vyetu kwa lengo la kutushirik-isha haya tuliojifunza," alisema Bw. Msilu.

Kamati ya Watumiaji wa Hudu- ma za Nishati na Maji mkoani Ru- vuma imejipanga kufikia makundi mbalimbali zaidi ya watumiaji, ya- kiwemo ya VICOBA ili kuhanakisha kuwa jamii ya Watanzania, hususani watumiaji wa huduma za nishati na maji wanapata elimu sahihi na uele- wa wa haki na wajibu wao kuhusu sekta hizi.



Tumia Mkandarasi Aliyesajiliwa

kufanya ukaguzi wa mtando wa nyaya (**Wiring**) kwenye jengo lako

kuondoa **upotevu** wa umeme na kujiongezea usalama!

Muda unaopaswa kuzingatiwa

Makazi ya kuishi	Majengo ya biashara	Viwanda	Majengo ya umma	Majengo mengine
				
Kila baada ya miaka 5	Kila baada ya miaka 4	Kila baada ya miaka 3	Kila baada ya miaka 3	Kila baada ya miaka 2

Kuona wakandarasi ingia: **nikonekt.tanesco.co.tz** au tumia Nikonekt App kisha chagua wakandarasi.

Tanga UWASA yapongezwa ubunifu wa hatifungani ya kijani



Mkurugenzi Mtendaji wa TANGA UWASA, Mhandisi Godfrey Hilly, akiwasilisha mada kuhusu hati fungani ya kijani mbele ya Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji walipotembelea mamlaka hiyo tarehe 24 Septemba 2024.

Na Nuru Zuberi, Tanga

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limeipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) kwa ubunifu wake wa hatifungani ya kijani.

Pongezi hizo zimetolewa hivi karibuni na Mwenyekiti wa EWURA CCC Mhandisi David Ngula, wakati wa ziara ya kitembelea Mamlaka hiyo ambayo ilijumuisha wajumbe wa Baraza, Sekretarieti na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Tanga.

Mhandisi Ngula alisema suala la kuanzishwa kwa hatifungani hiyo ni la kupongezwa, kwani litaongenza ufanisi wa Mamlaka katika kutoa huduma kwa wateja wake.

"Tunaipongeza Tanga UWASA kwa kufikiria ubunifu huu. Baraza linaamini miradi itakayofanyika kuititia hatifungani hii itaongeza upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira kwa wakazi wa Tanga ikiwemo ujenzi wa miradi ya miundombinu kama mtandao wa mabomba ya maji na matanki hasa maeneo yanayoguswa na mradi huu, kama

kata ya Ngamiani yaliyoko katikati ya mji," alisema Mha. Ngula.

Mhandisi Ngula alishauri Tanga UWASA kuelekeza pesa hizo kwenye miradi kama ilivyokusudiwa ili wananchi waweze kunufaika na hivyo Mamlaka hiyo kuzidi kutetea nafasi yake ya utendaji mzuri wa kazi kama ilivy kwenye taarifa za Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na ikibidi kurudi nafasi yake ya kwanza kama ilivyokuwa hapo awali.

"Ndugu zetu, pamoja na pongezi hizi lakini tunawasihi sana kuwa na mpango yakinifu katika kuhakikisha fedha hizi zinafanya kazi iliyokusudiwa, kwani hii itajenga uaminifu zaidi sambamba na kuwaweka katika nafasi nzuri zaidi kiutendaji," alisema Mhandisi Ngula.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Tanga UWASA Mhandisi Godfrey Hilly alieleza sababu kubwa ya kuwafanya kubuni mpango wa hatifungani ya kijani ni kutokana na Mamlaka kushindwa kufanya marejeo ya bei zake kwa zaidi ya miaka mitano, huku gharama za vifaa na dawa za kutibu maji kuendelea kupanda, lakini pia suala la uchakavu wa miundombinu.

Mhandisi Hilly alisema "wazo hili limetokana na changamoto amba zo tumekuwa tukabiliana nazozu na hivyo kuamua kuzigeuza kuwa fursa kwa kufikiria juu ya hatifungani ya kijani na tumefanikiwa kwa asilimia 103 mpaka sasa."

Aliongeza kwa kusema kupitia mradi huo Tanga UWASA in-adhamiria kuuza hatifungani kwa wateja ikiwa ni sehemu ya mikopo ya muda mrefu kwao kwa lengo la kupata fedha za utekelezaji kwenye miradi mbalimbali ikiwemo kurekebisha miundombinu ya huduma.

"Awali tulikuwa na changamoto ya malalamiko kwenye miundombinu lakini kuititia miradi ya fedha za hatifungani baadhi ya miundombinu inaendelea kuboreshwa na kupunguza malalamiko," alisema Mha. Hilly.

Naye Katibu Mtendaji wa EWURA CCC Bi. Stella Lupimo aliwapongenza Tanga UWASA kwa uthubutu wa kuanzisha hatifungani ya kijani kwa kuwa italeta unafuu kwa wateja na kuleta matumani katika huduma ya maji pindi miradi itakapokamilika.

"Niwaombe mkipata faida kubwa muone namna ya kuwapunguzia wateja gharama za huduma ili wengi waweze kumudu kuzitumia pasipo maumivu," alisema Bi. Lupimo huku akiwatachia kheri Tanga UWASA katika utekelezaji wa miradi kuititia hatifungani hiyo ya kijani.



Waahidi kuendeleza ushirikiano na Baraza

Na Brenda Magoma, Iringa

Wadau wa huduma za nishati na maji mkoani Iringa wameahidi kutoa ushirikiano wa dhati kwa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) katika kutekeleza majukumu yake ndani ya maeneo ya mkoa.

Ahadi hiyo imetolewa na Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Iringa Ndugu Godfrey Mafungu, baada ya kupata elimu kuhusu masuala ya huduma za nishati na maji wakati wa programu ya uelimishaji iliyofanywa na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Iringa ya EWURA CCC, chuongi kwake mapema mwezi Novemba 2024.

Katika programu hiyo, mada mbalimbali zilitolewa kama vile maa-na ya EWURA CCC na kazi zake, haki na wajibu wa mtumiaji ikiwa ni pam-oja na matumizi sahihi ya huduma za

nishati na maji na namna ya kuwasilisha malalamiko.

Akiongea baada ya kupata elimu hiyo Bw. Mafungu alilishukuru Baraza na kusema kuwa, wanafunzi wa Chuo hicho wataendelea kuwa mabalozi wa elimu hiyo nzuri na muhimu walijopata.

"Tunawashukuru kwa kutoa elimu hii kwa wanafunzi wetu. Ni tumaini letu kuwa, tutachangia kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa jamii inayowezza kudumisha matumizi bora ya nishati na maji. Tupo tayari sasa kupaza sauti tunapoona huduma hazikidhi vi-wango, lakini pia kuwajulisha wengine kuhusu umuhimu wa kuchukua hatua dhidi ya huduma mbovu ili kuhamashisa uboreshaji wake," alisema Bw. Mafungu.

Bw. Mafungu aliahidi kushirikiana na Baraza katika kutoa elimu na kuwa, wanafunzi wa Chuo chake watakuwa mabalozi katika kueneza elimu inayohusu huduma za nishati na maji, ili kila

Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Iringa, Ndugu Painetho Madembwe, akielezea majukumu ya Baraza kwa wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Iringa wakati wa ziara ya Kamati hiyo chuongi hapo mwezi Novemba 2024, iliyolenga kutoa elimu kwa wanafunzi na wakufunzi.

mtumiaji wa huduma hizo ajue haki na wajibu wake.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nisahti na Maji mkoani wa Iringa Bw. Painetho Madembwe alimshukuru Mkuu wa Chuo kwa kuwapatia nafasi ya kutoa elimu kwa wanafunzi na wakufunzi wa Chuo hicho, akieleza kuwa, hiyo ni fursa muhimu kwa Baraza katika kutekeleza moja ya majukumu yake ya kusambaza taarifa muhimu zenye maslahi kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji.

"Tunakushukuru sana Mkuu wa Chuo kwa kutupatia nafasi ya kutoa elimu kwa wakufunzi na wanafunzi wa Chuo chako. Baraza lina jukumu la kuhakikisha kuwa, taarifa muhimu zinazowahusu watumiaji wa huduma za nishati na maji wanazipata kwa wakati na usahihi unaostahili," alisema Bw. Madembwe.

Kamati ya Watumiaji ya EWURA CCC mkoani Iringa itaendelea na uelimishaji makundi mbalimbali ili watumiaji waweez kupata uelewa wa masuala muhimu yanayohusu nishati na maji.

Tunakushukuru sana Mkuu wa Chuo

“ kwa kutupatia nafasi ya kutoa elimu kwa wakufunzi na wanafunzi wa Chuo chako. Baraza lina jukumu la kuhakikisha kuwa, taarifa muhimu zinazowahusu watumiaji wa huduma za nishati na maji wanazipata kwa wakati na usahihi unaostahili

Msiweke mbele posho, zingatieni elimu

Na Theresia Mande, Singida

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na maji (EWURA CCC) lime-washauri watumiaji wa huduma za nishati na maji mkoani Singida kutokuweka mbele malipo ya posho wakati wa kupatiwa elimu badala yake wazingatie elimu na maarifa wanayopewa kuhusu huduma hizo.

Ushauri huo huo umetolewa hivi karibuni na Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoaa wa Singida (RCC) Bi. Everista Lucas, wakati wa utekelezaji wa programu ya uelimishaji kwa vikundi vya VICOBA vinavyosimamiwa na Taasisi ya SIME ambapo wakati wa programu hiyo baadhi ya wadau waliohudhuria walionesha nia ya kudai malipo ya kuhudhuria.

Bi. Lucas alisema kuwa, taasisi nyingi zimekuwa zikikwama kufikisha elimu muhimu kwa jamii kutokana na wananchi kudai malipo wakati wanapohudhuria semina au mikutano ambayo ina lengo la kuwajengea uwezo na uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

"Ni utamaduni mbaya ambao ume-jeneka mionganini mwetu kuwa mtu akikualika au ukimwalika kwa lengo la kukupatia elimu basi anatakiwa akulipe posho, kitu ambacho kinazorotesha jithiada za taasisi mbalimbali

katika kuwapatia elimu muhimu wananchi, ambayo ni kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla," alisema Bi. Lucas.

Alisema EWURA CCC imekuwa ikifanya jithiada kubwa ya kutoa elimu kwa jamii kuititia majukwaa mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha watumiaji wa huduma za nishati na maji wanapata elimu juu ya wajibu na haki zao za msingi wanazostahili kuzipata wanapotumia huduma hizo, japo kumekuwa na kikwazo cha madai ya posho.

"Tumekuwa tukipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa waandaji wa majukwaa mbalimbali yanayowaleta pamoja wananchi ambao ni watumiaji wa huduma za nishati na maji. Hata hivyo, kumekuwa na mahudhurio hafifu kutoka kwa wananchi, kwa kuwa hakuna posho ya kushiriki mafunzo hayo," alisema Bi. Lucas.

Bi. Lucas aliwashauri wadau hao kuacha utamaduni wa kufikiria posho tu, badala yake kuzingatia zaidi elimu wanayoipata na namna gani inaweza kuwasaidia katika kutatua changamoto zinazohusu huduma za nishati na maji ambazo zinawakabili.

Akizungumza baada ya programu hiyo Bi. Hadija Nyuha ambaye ni mwanakundi wa VICOBA Singida mjini alikiri kuwepo kwa utamaduni huo mbaya uliojengeka mionganini mwa jamii, kufikiria posho hasa pale wakiambiwa kuna wageni wanakuja ku-

wapatia elimu.

"Ni kweli kuna hii tabia kwenye jamii yetu, na tumezoeshwa kwa kuwa miaka ya nyuma kuna taasisi zilikuwa zinakuja kutupatia elimu na baada ya semina kuisha tulikuwa tunapewa posho. Hii imekaa kwenye akili zetu na imekuwa kama utamaduni kuwa ukipatiwa elimu unapewa na posho pia," alisema Bi. Nyuha.

Bi. Nyuha alisema kwa sasa wananchi wanatakiwa kubadilika na kuondokana kabisa na utamaduni huo kwani bila kubadilika wananchi wataendelea kukosa fursa nyingi za kupatiwa elimu muhimu inayogusa maisha yao ya kila siku.

Kwa upande wake Mchungaji Elia Muve, Mwenyekiti wa moja ya vikundi hivyo vya VICOBA aliunga mkono hoja hiyo kwa kusema kuna haja wananchi kubadilika na kupenda elimu ili kujiongezea maarifa ambayo yataapelekea kuboresha maisha yao, badala ya kufikiria zaidi fedha kutoka kwa waelimishaji.

"Hebu fikiria leo tumepeata elimu muhimu ambayo itatusaidia katika kupata haki zetu sisi kama watumiaji wa huduma za nishati na maji. Elimu hii ni zaidi ya fedha ambazo unatumia kwa muda mfupi sana. Kwa upande wangu nilikuwa sifahamu kuwa malalamiko yanayohusu huduma za nishati na maji yana taratibu zake za namna ya kutatuliwa. Awali nilidhani ukipata changamoto inayohusu huduma hizi basi unaipeleka kwa Mwenyekiti wa Mtaa au pengine unapeleka Polisi, lakini leo baada ya kupata elimu hii najua wapi pa kupeleka malalamiko yangu kwa utatuzi sahihi," alisema Mch. Muve.

Alisema kuwa, pamoja na changamoto za ugumu wa maisha lakini hali hiyo isifanye wananchi kudai pesa kwa kila jambo, kwani wakiendekeza masilahi binafsi itawafanya wakose maarifa muhimu, na hata kuingia kwenye gharama kubwa za maisha, mathalani kulipa bili kubwa za maji au gharama kubwa za matumizi ya umeme ikiwa hawana uelewa sahihi kuhusu matumizi ya huduma hizi.

"Ugumu wa maisha usitufanye kudai pesa kwa kila jambo, kwani masilahi binafsi yanawenza kutunyima maarifa muhimu na kuongeza gharama zisizo za lazima," alihimiza Mch. Muve huku akisisitiza umuhimu wa kujenga utamaduni wa kuwa na hamu ya kupata maarifa mapya badala ya kutanguliza pesa mbele.



Bw. Geofrey Sokesia, Afisa Huduma kwa Wateja EWURA CCC Singida (wa tatu kulia), akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani humu, pamoja na wanachama wa kikundi cha VICOBA, baada ya ziara yao kwa kikundi hicho kwa lengo la kutoa elimu kuhusu Baraza na majukumu yake.



TANESCO

www.tanesco.co.tz

Ndugu Mteja! 

Sasa unaweza kutoa taarifa ya hitilafu ya umeme katika eneo lako ndani ya

Mkoa wa Mara

kwa kutupigia katika nambari za simu zifuatazo

 **0748 550 000**
0735 165 088

Au kwa kutembelea ofisi zetu za TANESCO zilizopo jirani nawe.

[www.tanesco.co.tz](#)

#TupoKazini



KUWA
MZALENDO
TOA TAARIFA
UONAPO BOMBA
LA MAJI LIMEPASUKA


@IruwasaIringa

TUPIGIE


HUDUMA KWA MTEJA
0800 110 122



HabariPicha



Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Kagera Bw. Eustadi Katunzi, akitoa elimu na kugawa vipeperushi kwa washiriki wa Bonanza la Vijana kabla ya kuanza kwa michezo wakati wa Bonanza hili lililowakutanisha vijana kutoka maeneo mbalimbali mkoani humo.



Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Kagera, Bw. Najim Bwanika, akitoa elimu kuhusu majukumu ya Baraza kwa wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari Samia Suluhu (walimu hawapo pichani).



Bi. Bertha Maqway, Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Tanga (wa kwanza kushoto), akitoa elimu kwa watumiaji wa huduma hizo walitembelea banda la EWURA CCC, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari Usagara, Tanga, Agosti 12, 2024.

HabariPicha



Bw. Mrisho Mjinga, (Aliye simama) akitoa maoni yake mbele ya Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Singida (hawapo katika picha), wakati wa mkutano wa wanachi wa mtaa Mnung'una.



Afisa Huduma kwa Wateja EWURA CCC Pwani Bi. Noela Ntiluvakule akitoa elimu kuhusu huduma za nishati na maji kwa Wanachama wa vikundi vya wajasiliamali toka katika kata za wilaya ya Kibaha hivi karibuni



Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoaa wa Pwani Bi. Adela Kajuna akigawa vipeperushi kwa wanafunzi wa Chuo cha ufundi stadi Veta wakati wa programu ya uelimishaji uliofanyika chuongi hapo hivi karibuni.

Fahamu namna ya kuwasilisha malalamiko yako

Catherine Ochido, Ilala

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa kupitia kifungu cha 7 cha Sheria ya EWURA imepewa jukumu la kusimamia utatuzi wa malalamiko na migogoro kati ya watumiaji na watoa huduma, ili kutoa fursa ya haki kwa pande zote.

Pamoja na kuwa watumiaji wana haki ya kupatiwa huduma bora za nishati na maji, lakini pia wanao wajibu wa kulalamikia huduma mbovu kwani kufanya hivyo ni kuwakumbusha watoa huduma kuboresha huduma zao.

Ili kufanikisha utatuzi wenye ufanisi na haki kwa upande wa mtoya huduma na mtumiaji, kunaenda sambamba na kifungu cha sheria tajwa hapo juu, pamoja na Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Utaratibu wa Usuluhishi wa Malalamiko ya Watumiaji), 2020.

Kupitia Sheria na Kanuni hizo, EWURA imeweka utaratibu unaozingatiwa wakati wa kutatua migogoro inayojitokeza katika utoaji wa huduma za umeme, mafuta, gesi asilia na maji na usafi wa mazingira. Kanuni hizi zinalekeza namna ya kuwasilisha malalamiko

pamoja na utaratibu wa kushughulikia malalamiko.

Makala hii inalenga kuelezea utaratibu huo ili mtumiaji apatapo changamoto kuhusu huduma za nishati na maji ajue nini cha kufanya:

- Mtu mwenye malalamiko dhidi ya mtoya huduma za nishati na maji anaweza kuwasilisha malalamiko yake EWURA. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha sheria ya EWURA na Kanuni ya 4 ya Kanuni za EWURA za utaratibu wa kutatua migogoro.

- Mlalamikaji anatakiwa awe amewasilisha kwanza malalamiko hayo kwa mtoya huduma na iwapo hataridhika na hatua zilizochukulipa na mtoya huduma ndipo atawasilisha lalamiko lake EWURA.

- Malalamiko hayo yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya barua pepe, ambapo mlalamikaji atatakiwa kujaza fomu ya malalamiko ambayo inapatikana katika mfumo wa kielektroni wa LOIS katika tovuti ya EWURA.

- Kanuni ya 4(2&5) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro, 2020 inaipa EWURA CCC mamlaka kuwasilisha malalamiko kwa niaba ya watumiaji.

- Halikadhalika kikundi cha watu kinaweza kuwasilisha malala-

miko ilimradi yaambatane na orodha ya majina, saini au alama ya dole gumba na muhutasari wa kikao kilichoamua kuwasilishwa kwa malalamiko hayo EWURA. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 4 (4) ya Kanuni tajwa hapo juu.

- Pamoja na utaratibu huu, Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi linalelekeza kuwa mlalamikaji anatakiwa kuweka wazi taarifa zifuatazo;

- a. Jina/majina.
- b. Jina la mwakilishi (kama ni tofauti na anayelalamika)
- c. Namba ya akaunti ya huduma husika
- d. Anuani ya posta
- e. Namba ya simu
- f. Taarifa za anayelalamikiwa na anuani yake
- g. Aina ya malalamiko
- h. Nakala za nyaraka kuhalalisha malalamiko husika

Jinsi EWURA inavyoshughulikia malalamiko;

- Baada ya malalamiko kupokelewa, EWURA huwasiliana na mlalamikaji ili kumpelekeea malalamiko husika, ambapo atatakiwa kuwasilisha utetezi wake ndani ya siku 21.

- Baada ya kupokea utetezi wa mlalamikaji EWURA huitisha kikao cha kutafuta muafaka ikiwi ni sehemu ya uchunguzi wa kuzisaidia pande husika kufikia makubaliano.

- Iwapo hakuna makubaliano yaliyofikiwa shauri hupelekwa mbele ya Kamati maalum ya EWURA kwa ajili ya kusikilizwa na pande husika hupata fursa ya kujieleza na kutoa ushahidi.

- Baada ya shauri kusikilizwa, Kamati hiyo hupelekwa mapendekezo kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA ambayo hufanya uamuzi na kutoa tuzo (Award), ambapo uamuzi wa Bodi ya EWURA una nguvu sawa na amri ya Mahakama kuu.

- Iwapo upande wowote haujaridhika na uamuzi wa EWURA, unaweza kukata rufaa kwenye Baraza la Ushindani (Fair Competition Tribunal) ndani ya siku 21 tangu kupokelewa kwa uamuzi uliotolewa na Bodi ya EWURA.

EWURA CCC inawahimiza watumiaji kufuata taratibu hizi ili kuhakikisha malalamiko yao yanashughulikiwa kwa ufanisi na uwazi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.



Mtu mwenye malalamiko dhidi ya mtoya huduma za nishati na maji anaweza kuwasilisha malalamiko yake EWURA. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha sheria ya EWURA na Kanuni ya 4 ya Kanuni za EWURA za utaratibu wa kutatua migogoro



Bw. Victor Baguma, Mwezesaji wa Mafunzo kutoka Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP), akitoa maelezo kuhusu ujenzi wa bomba la mafuta kwa Ujumbe wa Baraza ulioongozwa na Mwenyekiti wake, Mha. David Ngula, ulipotembelea eneo la Mradi mkoani Tanga, Septemba 2024.

Hongera EACOP kwa kushirikisha jamii - Ngula

Na. Nuru Zuberi, Tanga

Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) Mha. David Ngula amepongeza Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi Afrika Mashariki (The East African Crude Oil Pipeline Project (EACOP)) katika kushirikisha wananchi wa Chongoleani linakopita bomba la Mradi huo, huku ukizingatia masuala ya mazingira na afya kwa jamii.

Mha. Ngula ametoa pongeza hizo alipoongoza Ujumbe wa Baraza ulio-jumuisha Wajumbe wa Baraza, wafanyakazi wa Baraza na Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji ya Baraza Mkoani Tanga, katika ziara ya kutembelea Mradi huo iliyo-fanyika Septemba 25, 2024.

Ngula alieleza kufurahishwa kwake na namna Mradi huo unavyo-

oshirikiana na jamii hususani wakazi wa Chongoleani katika kuhakikisha kuwa, shughuli za ujenzi na operesheni zingine hazileti madhara yoyote kwa mazingira na kwa afya za wananchi wa eneo hilo.

"Ni furaha kubwa kuona jinsi Mradi huu unavyohusisha wananchi katika shughuli zake kwa kutoa taarifa na kuwahusisha katika michakato ya maamuzi. Hii ni ishara ya uwazi na utawala bora. Vilevile tunapongeza hatua zinazochukuliwa za kuhakikisha kwamba mazingira yanahifadhiwa na afya za watu zinazingatiwa," alisema Mha. Ngula.

Aidha, alieleza kuwa, Mradi huo umekuwa ulkitoa mafunzo na fursa za ajira kwa vijana wa eneo la Chongoleani, jambo ambalo limeongeza ustawi wa jamii na kuleta manufaa ya kiuchumi kwa wananchi hao.

Ngula alisitisiza juu ya umuhimu wa ushirikiano wa pande zote zin-

azohusika katika Mradi huo ili kuhakikisha kuwa unakuwa chachu ya maendeleo kwa jamii bila kuleta madhara kwa wanadamu na viumbe vingine vya asili katika eneo hilo.

"Tunaamini kuwa maendeleo haya ni muhimu, lakini pia tunapaswa kuhakikisha kuwa tunalinda mazingira yetu kwa ajili ya kizazi kilichopo na kijacho," alisema Mha. Ngula.

Naye Msimamizi wa Mahusiano wa Mradi huo wa EACOP Bw. Daniel Semkiwa alieleza kuwa, EACOP itaendelea kushirikiana na jamii kwa kuhakikisha kuwa miradi yao inazingatia viwango vya kimataifa vya usalama wa mazingira na afya za watu.

Aliongeza kuwa, Mradi huo una mikakati ya kudumu ya kutoa msaada kwa jamii, ikiwa ni pamoja na miradi ya afya, elimu na maendeleo ya kiuchumi.

Ziara hii ya Baraza inakuja wakati ambapo Mradi wa EACOP unakaribia kukamilika na unatarajiwa kuwa na matokeo chanya kwa uchumi wa nchi za Afrika Mashariki, hasa katika sekta ya nishati ambapo bomba hilo la mafuta linalengwa kufungua njia ya usafirishaji wa mafuta ghafi kutoka Uganda hadi bandari ya Tanga Tanzania, ambapo yatauzwa katika soko la kimataifa.

Gesi Asilia: Mkombozi nishati safi kwa kaya Tanzania

Na Saidi Ismail, Mtwara

Katika juhudzi za kuboresha maisha na kulinda mazingira, gesi asilia imekuwa suluhisho muhimu la nishati safi kwa kaya nyingi nchini Tanzania, kwani inapunguza matumizi ya kifedha kwa kiasi kikubwa.

Faida kubwa ya gesi asilia

Kwa sasa, gesi asilia inachukuliwa kama mbadala wa nishati zenyе changamoto kama mkaa, na kuni. Ikilinganishwa na nishati hizo, gesi asilia ni nafuu zaidi, inapatikana kwa urahisi kupitia mifumo ya mabomba, na haina moshi unaochafua mazingira au kuathiri afya.

Faida zingine za gesi asilia ni kama ifuatavyo:-

Gharama Nafuu

Gesi asilia ni chaguo lenye unafuu mkubwa kwa kaya, ikipunguza matumizi ya nishati ghali kama kuni, mkaa na LPG (Liquefied Petroleum Gas) kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, Bi. Halima Saidi, mkazi wa mtaa wa Reli, Mtwara Mikindani, amepunguza matumizi yake ya kifedha kutoka shilingi 30,000 kwa mwezi kwa ununuza wa mkaa hadi shilingi 10,000 hadi 15,000 kwa uniti za gesi asilia.

Usambazaji wa moja kwa moja

Tofauti na LPG inayohitaji mitungi, au kuni na mkaa, gesi asilia husambaza

zwa moja kwa moja hadi majumbani kupitia mabomba, hivyo kupunguza changamoto za uhifadhi.

Rafiki wa mazingira

Nishati hii hutoa uchafuzi mdogo wa hewa ikilinganishwa na mkaa na mafuta. Hii inasadia kulinda mazingira na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ufanisi

Gesi asilia inatoa joto la haraka na rahisi kudhibiti, hivyo kusaidia kuo-ko muda wakati wa kupika.

Tofauti katи ya Gesi Asilia na LPG

LPG hutokana na kuchakata mafuta ya petroli na inajumuisha gesi za propane na butane. Hutumiwa kwa matumizi ya kupikia, viwandani, n.k. Hata hivyo, hufanya kazi tofauti na gesi asilia (Natural Gas), ambayo hutolewa moja kwa moja ardhini na kusambazwa kupitia mabomba.

Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Nishati ya 2015, Serikali inapendekeza matumizi ya nishati safi kama gesi asilia badala ya kuni na mkaa ili kupunguza uharibifu wa mazingira na athari za kiafya kwa wananchi kuto-kana na moshi wa kuni.

Maendeleo ya usambazaji wa Gesi Asilia Tanzania

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limefanikiwa kuanzisha miradi ya kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam,

Mtwara na Lindi. Hadi sasa, zaidi ya kaya 520 zimeunganishwa na mtando wa gesi asilia katika maeneo haya. Katika jiji la Dar es Salaam, mfumo huu umepunguza uchafuzi wa hewa unaosababishwa na matumizi ya mkaa.

Kwa mikoa ya Mtwara na Lindi, ambapo gesi asilia inazalishwa kwa wingi, jamii zimeanza kufurahia nishati hii kwa gharama nafuu. Aidha, matumizi ya gesi asilia yamekuwa msaada mkubwa mashulenii na kwenye taasisi nyingine zinazohitaji nishati nyingi kwa ufanisi.

Jukumu la EWURA CCC

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limekuwa likihamasisha matumizi ya gesi asilia kupitia kampeni zake za uelimishaji. Semina mbalimbali zinazohusiana na usalama na faida za gesi asilia zimekuwa zikifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, na Lindi, ambapo mfumo wa gesi umeshaanza kufanya kazi.

EWURA CCC inahakikisha watumiaji wanapata taarifa sahihi kuhusu usambazaji wa gesi na namna ya kuitumia kwa usalama na usahihi. Hii inalenga kupanua uelewa wa jamii juu ya faida za nishati safi na kupunguza utegemezi wa nishati zenyе athari mbaya kwa mazingira.

Gesi asilia ni chachu ya mabadiliko katika sekta ya nishati Tanzania. Kupitia usambazaji wa moja kwa moja na gharama nafuu, inaboresha maisha ya watu wa kawaida, kupunguza athari za kiafya na kimazingira, huku ikiimarisha uchumi wa kaya.



Zingatia haya katika kukata rufaa

Na Neema Nnko, Manyara

Ie, unafahamau muda sahihi wa kukata rufaa juu ya migogoro inayoweza kujitokeza kati ya watumiaji wa huduma za nishati na maji dhidi ya watoa huduma hizo? Je, unafahamu sababu zinazotambulika na ambazo zitafanya rufaa yako kusikilizwa?

Makala hii itaangazia muda ambaao mtumiaji wa huduma za nishati na maji anaweza kukata rufaa juu ya uamuzi wa shauri au lalamiko linalohusiana na huduma za nishati na maji endapo hakuridhika na uamuzi uliotolewa na EWURA wakati wa kusikilizwa kwa lalamiko lake.

Makala pia inaangazia sababu zinazoweza kusababisha upande fulani kukata rufaa hiyo na pia kufahamu sababu zitakazofanya rufaa kukubalika na lalamiko kufanyiwa kazi tena upya. Ni muhimu kwa mtumiaji kufahamu hatua hizi ili akipatwa na changamoto hizi afahamu hatua za kuchukua ili kupata haki yake.

Kanuni za Kutatua Malalamiko za EWURA za Mwaka 2020 (The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Consumer Complaints

Settlement Procedure) Rules, 2020) ni mionganini mwa nyenzo muhimu zinazotumika kuongoza mchakato wa kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya EWURA. Kanuni hizi zinalenga kutoa mfumo wa utatuvi wa malalamiko kwa njia ya haki, uwazi na ufanisi.

Muda wa kukata rufaa

Kanuni ya 23 ya Kanuni tajwa hapo juu inaeleza kuwa upande ambaao haukuridhika na uamuzi wa EWURA chini ya Kanuni ya 21 unaweza kukata rufaa kwenda Baraza la Ushindani (FCT) ndani ya siku 21 kutoka tarehe ya kutolewa kwa tuzo.

Rufaa hii ni lazima izingaties misingi au sababu ya kukata rufaa kama ilivyyoainishwa kwenye Kanuni ya 24(a-d) ya Kanuni kwamba, mtu ye yeyote anaweza kukata rufaa endapo maamuzi ya tuzo hayakuzingatia yafuatayo: -

a. Tuzo iliyotolewa haikuzingatia/haikutegemea ushahidi uliowasilishwa na mlalamikaji. Hii inajumui-sha uamuzi ambaao hauendani na ushahidi uliotolewa, au uamzi ambaao haupo katika mipaka ya sheria. Inahu halii ambapo uamuzi wa awali

unadhihirisha kuwa haukuwa na mantiki na haukuzingatia vigezo ya haki.

b. Uamuzi ultolewa kwa makosa ya kisheria. Hii inahusiana na matumizi mabaya ya sheria au kutotumika kwa sheria inayohusiana na malalamiko ya mtumiaji. Mfano, kama Kamati au Mamlaka ilikosea kutafsiri au haikutumia sheria ipasavyo.

c. Taratibu au masharti mengine ya kisheria yanayohusiana na mamlaka hayakufuatwa na kutokufuata taratibu hizo uliathiri maamuzi yaliyotolewa. Misingi hii inahusisha ukiukaji wa taratibu zilizowekwa za kisheria au kiutawala wakati wa kusikiliza malalamiko. Hii inaweza kumaanisha kutofuatwa kwa mchakato wa kisheria wakati wa uchambuzi wa malalamiko ya mtumiaji.

d. Mamlaka haikuwa na uwezo wa kutoa tuzo. Hii inamaanisha kuwa maamuzi haya yaliyotolewa na mamlaka hayakupaswa kutolewa na mamlaka hiyo na kwamba yalipaswa kutolewa na chombo kingine chenye mamlaka ya juu zaidi kutokana na aina ya lalamiko lilokuwa linashughulikiwa.

Rufaa inazo faida mbalimbali kwa mlalamikaji au mlalamikiwa ikiwa hajaridhika na maamuzi ya EWURA.

Kwanza, FCT hutoa fursa ya kuititia upya na kutathmini kwa kina uhalali wa maamuzi yaliyotolewa, ikizingatia ushahidi na hoja zote zinazohusiana. Hii inasaidia kuhakikisha kuwa haki imetendeka na maamuzi hayakufanyika kwa upendeleo au makosa ya kisheria.

Pili, FCT ni chombo huru amba-cho hutoa nafasi ya pili kwa wahusika kupata suluhu, hasa pale ambapo wanahisi kuwa maslahi yao hayakuzingatiwa ipasavyo na EWURA.

Aidha, rufaa inaweza kusababisha mabadiliko ya maamuzi, fidia, au hatua nyingine zinazoweza kunufaisha pande zote, na pia huchangia kuboresha uwajibikaji na uwazi katika utoaji wa huduma. Hatimaye, ni njia muhimu ya kudumisha imani ya umma kwa mifumo ya udhibiti wa huduma na haki za watumiaji.

Baraza litaendelea kutoa elimu mbalimbali kwa watumiaji kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika mustakabali mzima wa kujenga Taifa lenye wananchi wenye uelewa mpana kuhusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.

Makala

Hatua za usalama katika vituo vya kujaza gesi asilia Iliyogandamizwa

Na Sakina Yusuf, Tabora

Gesi asilia iliyogandamizwa (Compressed Natural Gas (CNG)) imekuwa chanzo muhimu cha nishati katika miaka ya hivi karibuni barani Afrika, kutokana na urafiki wake kwa mazingira na unafuu wa gharama kwa watumiaji wa vyombo vya moto. Kwa Tanzania huduma hii inapatikana kwa wingi katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Hata hivyo, usalama katika vituo vya kujaza CNG ni suala muhimu sana linalohitaji kutiliwa mkazo katika kufuata taratibu zilizowekwa ili kuepusha madhara kwa mtumiaji na jamii kwa ujumla.

Kanuni ya 39(1)(2) ya Kanuni za Mafuta (Gesi Asilia Iliyogandamizwa) (Huduma za Ugavi na Masoko) za Mwaka 2019 zimeweka wazi juu ya usalama wa mteja na alama za usalama ili kuhakikisha kuwa vituo vya kujaza CNG vinatumika kwa usalama.

Kanuni ya 39 (1) ya Kanuni tajwa, inaelekeza kuwa, mto huduma atafuata sheria zote zinazohusu usalama wa mteja na alama za taarifa katika kituo

chake. Sambamba na hiyo, Kanuni ya 39 (2) inamtaka mto huduma kuhakikisha usalama katika vituo vya kujaza CNG kwa kuonyesha ishara muhimu katika maeneo yanayofaa Ishara hizo ni pamoja na:

1. Bango la kuonesha bei: Bango hili linapaswa kuwa wazi na rahisi kusomeka, ikionesha bei ya sasa ya gesi alisia iliyokandamizwa (CNG).

2. Onyo la kuzima simu: Kuto-kana na hatari ya moto unaoweza kusababishwa na simu za mkononi, ni muhimu kuwa na ishara inayoonya wateja kuzima simu zao wakati wa kujaza gesi.

3. Onyo la kutowuta sigara: Sigara zinaweza kusababisha moto, hivyo ni muhimu kuwa na ishara inayozuria kuvuta sigara katika eneo la kituo cha kujaza gesi.

4. Onyo la kuzima injini: Injini zinazofanya kazi zinaweza kusababisha cheche ambazo zinaweza kuwashaa gesi, hivyo ni muhimu kuzima injini wakati wa kujaza gesi.

5. Ishara zingine za usalama: Kulingana na mahitaji ya sheria, kuna weza kuwa na ishara nyingine za usalama ambazo zinahitajika kuoneshwa

ili kuwalinda watumiaji.

Je kuna umuhimu gani kufuata kanuni hizi?

Kufuata kanuni hizi kwa mto huduma kunahakikisha usalama wa wateja, wafanyakazi na watumiaji wengine wa huduma katika kituo hicho. Kwa kuzingatia mahitaji haya, hatari ya moto, mlipuko au ajali nyingine zinazohusiana na gesi zinaweza kuepukwa kwa kiasi kikubwa.

Je ni nini wajibu wa watumiaji?

Wateja na wafanyakazi wa kituo pia wanapaswa kuchukua tahadhari zote za usalama. Wateja wanapaswa kufuata maelekezo yote yaliyotolewa na wafanyakazi wa kituo, na kuzingatia ishara zote za usalama ili kulinda afya na mali zao.

Usalama katika vituo vya kujaza gesi asilia iliyogandamizwa ni jambo la msingi. Kwa kufuata sheria na kanuni zilizowekwa, na kwa kushirikiana kwa karibu kati ya wamiliki wa vituo, wafanyakazi na wateja, tunaweza kuhakikisha kuwa matumizi ya CNG yanaendelea kuwa salama na ya manufaa kwa jamii nzima ya Kitanzania.



Picha inayoonesha moja ya kituo cha CNG kikitoa huduma kwa mteja.
Picha kwa hisani ya tovuti ya gnvmagazine.com



DUWASA kupunguza mgao wa maji Dodoma

Na Amani Mbogo

Mamlaka ya Majisafi na Usafifi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) imeahidi kupunguza mgao wa huduma ya maji ndani ya Jiji la Dodoma baada ya kuanza kutekeleza miradi mikubwa ya maji ili kuboresha huduma hiyo.

Ahadi hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Aron Joseph wakati wa ziara ya Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) ofisini kwake na vyanzo mbalimbali vya maji vya DUWASA, Novemba 19, 2024.

Mkurugenzi huyo aliezeza ujumbe wa Baraza uliiongozwa na Mwenyekiti wake Mhandishi David Ngula kuwa, mahitaji ya maji kwa jiji la Dodoma ni lita milioni 149 kwa siku, lakini uzalishaji kwa sasa ni lita milioni 71 tu, hivyo kufanya kuwa na upungufu ambaao unasababisha huduma hiyo kutolewa kwa mgao.

Mha. Joseph alitaja miradi inayotekeliza kwa lengo la kupunguza mgao

wa maji jijini Dodoma kuwa ni pamoja na mradi wa Nala ambaao utagharimu fedha za Kitanzania shilingi bilioni 1.5 kwa awamu ya kwanza ambapo hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 80 na kuwa utaanza kutoa huduma kwa wananchi haraka iwezekanavyo.

"Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya muda mfupi na mrefu lengo likiwa ni kuhakikisha inapunguza adha ya upatikanaji wa huduma ya maji katika jiji la Dodoma. Mradi wa Nala tayari umefikia asilimia 80 na wananchi wataanza kupata huduma haraka iwezekanavyo. Mradi mwengine ni wa wa Ihumwa, Njedengwa ambaao umegharimu fedha za Kitanzania shilingi bilioni 2.7 ambaao pia umekamilika kwa asilimia 100, na tayari umeanza kutoa huduma kwa wananchi," alisema Mha. Joseph.

Alisema kukamilika kwa miradi yote hiyo kutasadia kwa kiasi kikubwa kupunguza adha ya muda mrefu ya upatikanaji wa huduma ya maji katika jiji la Dodoma.

Mha. Joseph aliendelea kueleza kuwa, DUWASA inaendelea kutekele-

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafifi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) Mhandisi Aron Joseph akiwaeleza Wajumbe wa Baraza mipango ya Mamlaka hiyo katika kupunguza uhaba wa maji walipotembelea katika ofisi hizo, hivi karibuni.

za mradi wa Nzuguni awamu ya pili ambapo sasa upo katika hatua za manunuzi na mradi huo unatarajia kuongezea maji mengi zaidi kwa vyanzo viliviyopo sasa.

Alisema mradi huo ukikamilika utaondo kabisa mgao wa maji kwa wananchi wa maeneo ya Meriwa, Ilazo, Ipagala, Area C na Area D.

"Pia tunaendelea na ujenzi wa Bwawa la Farkwa, fedha za ujenzi wa awamu ya kwanza zimeshatikana, lengo letu ni kuhakikisha ifikapo Machi 2025 mkandarasi awe eneo la mradi akiendelea na kazi," aliongeza Mha. Joseph.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa EWURA CCC Bi. Stella Lupimo alisema, Baraza baada ya kutembelea miradi na vyanzo vya maji vya DUWASA, Wajumbe wa Baraza wameridhishwa na namna Mamlaka hiyo inavyotekeliza majukumu yake, na mipango iliyopo ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji jijini Dodoma.

Inaendelea Uk. 22

Inatoka Uk. 21

Alisema Dodoma inakua kwa kasi na mahitaji ya maji yanakua, hivyo ni matumaini ya Baraza kuwa, katika mipango ya DUWASA itaangalia takwimu za ongezeko la idadi ya watu ili kuwa sambamba na mikakati endelevu ya otoaji huduma ya maji inayoendana na takwimu halisi.

"Tumevutiwa na utekelezaji wa majukumu ya DUWASA na mipango yao ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji jijini Dodoma. Dodoma inakua kwa kasi na mahitaji ya maji yanazidi kuongezeka, hivyo ni matumaini ya Baraza kuwa DUWASA itazingatia takwimu za ongezeko la idadi ya watu katika mipango yake ili kutatua changamoto ya ubaha wa maji kwa njia inayolingana na hali halisi ya ongezeko la idadi ya watu," alisema Bi. Lupimo. Hata hivyo Bi. Lupimo alitoa wito kwa watumiaji wa huduma ya maji jijini Dodoma kutunza miundombinu ya maji ili kuwa na

DUWASA kupunguza mgao wa maji Dodoma

huduma endelevu.

"Tunatoa wito kwa watumiaji wa huduma za maji zinazotolewa na DUWASA kuhakikisha wanaendelea kutunza miundombinu ya maji ili huduma hizi ziweze kuwa endelevu," alisema Bi. Lupimo.

Akitoa shukrani kwa Uongozi wa DUWASA, Mwenyekiti wa EWURA CCC, Mhandisi David Ngula alisema kuwa, wameona namna DUWASA walivyojipa kuhakikisha watumiaji wanapata

huduma ya maji kikamilifu.

"Kwa kweli Baraza tumeona njia mnazozitumia kuhakikisha wateja wote wanapata huduma ya maji iliyobora na ya kuaminika, na pia tunaamini kwa jitihada mnazofanya mtaweza kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wateja wenu wote, ikiwa ni pamoja na kushughulikia kwa wakati malalamiko yanayojitekeza kutokana na huduma zenu," alihitimisha Mha. Ngula.

Baraza lilifanya ziara hiyo kwa lengo la kujionea miradi inayotekelvezwa na DUWASA lakini pia kujionea namna Mamlaka hiyo inavyofanya kazi, changuamoto wanazokutana nazo pamoja na mipango walivyonyo kwa ajili ya kuboresha huduma za maji katka jiji hilo linalokuka kwa kasi.

Ujumbe huo wa Baraza ulijumuisha Wajumbe wa Baraza, wafanyakazi wa Baraza, pamoja na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati ya EWURA CCC mkoani Dodoma.



**Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa
Mazingira Tabora
(TUWASA)**



**WAUNGWANA HUANZA WIKI
KWA KULIPA ANKRA KWA
WAKATI**



JE WEWE NI MIONGONI MWAO..??

"Kuwa Muungwana lipa bili yako sasa"

0800780063  tuwasatabora.3 @ tuwasa_tabora  www.tuwasa.go.tz



Walalamikia ukosefu wa maji Mawanjeni

Na Zamda Mabada, Kilimanjaro

Wakazi wa Kijiji cha Mawanjeni kilichoko Kata ya Mwika Kusini, Wilaya ya Moshi, wamelalamikia tatizo la ukosefu wa huduma ya maji kwa muda mrefu na kusababisha kutafuta huduma hiyo kwa gharama kubwa huku wakihofia usalama wa afya zao kutokana na maji wanayonunua kutoka kwenye vyanzo visivyoaminika.

Haya yameibuka hivi karibuni wakati Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya EWURA CCC mkoani Kilimanjaro ikitekeleza programu za uelimishaji katika maeneo mbalimbali ya Kata hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wa Kitongoji cha Liata Kijiji cha Mawanjeni, Mwenyekiti wa Kitongoji hicho Bw. Rashidi Saidi Mfinanga alieleza kuwa, hali hiyo imedumu kwa muda mrefu kiasi cha kufanya wananchi wa eneo lake kupata huduma ya maji kwa gharama kubwa, lakini pia kutumia maji ambayo usalama wake kiafya ni mdogo.

"Tunaomba Mamlaka ya Maji itupatie huduma ya maji ndani ya kijiji chetu kama walivyotuhidi wakati wanakabidhiwa na jumuiya ya maji ya Kili Water. Tunatumia gharama kubwa sana kununua maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya nyumbani huku tukiwa hatuna uhakika na usalama wa maji hayo," alisema Bw. Mfinanga.

Kwa upande wake Bi. Rose Uriro mkazi wa Kitongoji cha Karango "B" alieleza kusikitishwa kwake na hali ya kukosa huduma muhimu ya maji

kwa muda mrefu, ingawa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA) iliahidi kuwaaletea huduma hiyo wakati ilipokabidhiwa kuhudumia eneo hilo mwaka 2017.

"Kinachoniuma ni kuwa, hata miundombinu ya maji tulifunga kabisa kwa gharama zetu, ikiwemo kuchimba mitaro lakini mpaka leo hii tunanunua maji kwenye madumu, tena kuto-ka kwenye vyanzo visivyoaminika," alilalamika Bi. Uriro.

Joakim Urassa mkazi wa Kitongoji cha Karoro ni mionganini mwa watu walipopaza sauti zao huku akiionba MUWSA kuchukua hatua stahiki na ya hataka ili waweze kuondokana na adha hiyo.

"Nawasihi MUWSA kuchukua hatua stahiki na za haraka kuhakikisha huduma hii inapatikana kwetu, kwani hatuna uhakika wa maji safi na salama ya kutumia. Naomba waongeze jitihada za kuondoa tatizo hili hata kwa kuchimba visima na kutusambazia maji ili kuondoa adha ya kununua maji yasinyokuwa na uhakika na usalama," alisema Bw. Urassa.

Baada ya kupokea malalamiko hayo, Ofisi ya Baraza mkoani Kilimanjaro iliwasilisha kwa mtoa huduma na kuomba kupata ufanuzi kuhusu changamoto hiyo inayowakibili wananchi hao.

Akitolea maelezo kuhusu lalamiko hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa MUWSA Mhandisi Innocent Lugodisha alieleza kuwa, changamoto hiyo inasababishwa na uchache wa vyanzo vya maji na kukosa miundombinu ya kutosha kusambaza maji katika eneo hilo.

Alieleza kuwa, baada ya Mamla-

Bi. Rose Uriro, mkazi wa Karango B, Kijiji cha Mawanjeni, Kata ya Mwika Kaskazini, Wilaya ya Moshi, akiwasilisha malalamiko kuhusu ukosefu wa huduma ya maji kwa Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC Kilimanjaro (hayupo pichani), katika mkuu wa wananchi uliofanyika Oktoba 2024.

ka kukabidhiwa kuhudumia maeneo hayo kutoka kwa "Jumuiya ya Maji ya Kili Water," ilikuta miundombinu inayotumika imechakaa lakini pia ilikuwa hajatandazwa eneo kubwa la kijiji hicho.

"Changamoto hii tumeiona na iko katika vitongoji vya Mawanjeni na Liata ambako miundombinu ya mabomba imepita mbali. Mkakati tulionao kwa sasa ni kuanza kutanda za mabomba upya kwenye maeneo hayo ambayo yanatumia chanzo cha Kyaronga. Kwa sasa baadhi ya maeneo ya Mwika Kaskazini yanapata maji ya kutosha na maeneo mengine yanapata kwa uchache," alisema Mha. Lugodisha.

Aliendelea kueleza kuwa, mpango mkakati mwinge ni wa kuchimba visima ili kusambaza maji kwenye maeneo ya Mwika Kaskazini ambapo maji yanaonekana hayatoshelezi.

Mha. Lugodisha alieleza pia kuwa kwa kufanya hivyo anamini watakuwa wametutua kwa kiasi kikubwa changamoto ya uhaba wa maji katika eneo hilo.

Ufutiliaji wa Baraza pia umebaini kuwa, timu ya maafisa wa MUWSA tayari imefika katika eneo lenye changamoto na kuwasiliana na uongozi wa Kijiji kufanya uchunguzi na tathmini ya utatuza wa changamoto hiyo kama ilivyoahidiwa.

Ofisi ya Baraza mkoani Kilimanjaro itaendelea kufutilia ili kuhakikisha kero hii inakwisha kabisa.

HabariPicha



Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Pwani akiwakwenye zoezi la kutoa elimu na kugawa viepeperushi vya Baraza kwa wateja na wafanyabiashara ya nyama katika Machinjio ya wanyama ya Loliondo Walayani Kibaha.



Bi. Doris Elijah, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji Pwani, akitoa elimu kuhusu huduma za nishati na maji kwa wananchi walitembelea banda la EWURA CCC katika Maonesho ya Nne ya Biashara na Uwekezaji, yaliyofanyika kwenye viwanja vya stendi ya zamani, Mailimoja, Kibaha, kuanzia tarehe 16 hadi 20 Desemba 2024.



Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC Ruvuma Bi.Magreth Temba akitoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya huduma za Nishati na Maji kwa Wanafunzi wa shule ya Msingi Miembeni iliyopo Manispaa ya Songea..



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
MOSHI (MUWSA)



Matangazo

LIPA ANKARA
YAKO **KWA**
WAKATI

Ili uendelee kufurahia
huduma zetu kupitia,



WAKALA WA **BENKI**



 muwsa  moshi_muwsa  Mamlaka ya majisafi Moshi  Majimoshi

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TANGA
(TANGA UWASA) 
"ISO 9001:2015"



#TANGAUWASA_UPDATES SEP 5, 2024

**TANGA UWASA YAENDELEA NA ZOEZI LA
UFUNGAJI WA MITA ZA PREPAID MWAKIZARO.**

 @tangauwasa

0800110111 Bure  0735 800 111

Kda Tone Lina thamani

Wanakwaya waaswa kuhamasisha haki na wajibu

Na Magreth Temba, Ruvuma

Wanakwaya wa Kwaya ya Mt. Don Bosco Parokia ya Mathias Mulumba Kalemba Jimbo Kuu Katoliki Songea wameaswa kuitumia kwa vitendo elimu waliyoipata kuhusu huduma za nishati na maji ikiwemo kuzingatia haki na wajibu wao.

Wito huo umetolewa hivi karibuni na Bi. Happy Sanga ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Ruvuma wakati Kamati hiyo ilipotembelea na kutoa elimu kwa wanakwaya hao.

Wanakwaya hao walielimishwa kuhusu haki na wajibu wao, ikiwemo haki ya usalama na faragha, ambapo walijulilishwa kuwa wana haki ya kuhudumiwa kwa faragha na kuhifadhiwa siri, kupata huduma iliyo salama na haki ya kudai fidia kutokana na hasara iliyosababishwa na mtohuduma.

Elimu nyingine iliyotolewa ni kuhusu wajibu wa mtumiaji, ikiwemo kuwa na matumizi halali ya huduma kwa kuzingatia taratibu zote za kisheria wakati wote ili kupata huduma zinazohusika na kutunza miundombinu ili kuwa na matumizi endelevu.

Wanakwaya hao pia walielimishwa kufahamu tofauti iliyoipata kati ya EWURA na EWURA CCC, ambapo waliezwa kuwa EWURA CCC ni Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji lililoanzishwa chini ya kifungu cha 30 cha Sheria ya EWURA, Sura Namba 414, kwa lengo la kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji. Lakini EWURA ni Mam-laka ya Udhhibit wa Huduma za Nishati na Maji, ikiwa na wajibu wa ku-simamia shughuli zote za kiuchumi na kiufundi katika sekta za nishati (umeme, petroli na gesi asilia) pamoja na maji (majisafi na usafi wa mazingira).

Pia, kikundi hicho cha wanakwaya kilifundishwa kuzifahamu Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira za Mwaka 2020, Tangazo la Serekali Na.849, ambapo, pamoja na mambo mengine, Kanuni ya 34(3) ya Kanuni hizo inazitaka mamlaka za maji zilizopewa leseni kufikia viwango vya kutoa huduma na kwamba kushindwa kufikia viwango vya ubora wa huduma zitawajibika kulipa fidia kwa waathirika. Lengo likiwa ni kuhakikisha watumiaji hawa wanakuwa na uelewa mpana zaidi utakaowasaidia katika matumizi yao ya kila siku ya huduma za maji.

Bi. Sanga aliwaomba wanakwaya hao kuwa mabalozi kwa kusambaza elimu hiyo kuptitaa jukwaa lao la uimbaji wa nyimbo za injili akiamini kuwa wanakwaya ni mionganoni mwa jamii inayotumia huduma za nishati na maji lakini pia uimbaji ni jukwaa mojawapo la kutoa elimu.

"Tunaamini kuwa elimu mliyopata mtaenda kuitumia vyema kwa maslahi yenu binafsi na kwa faida ya jamii inayowazunguka kwani uimbaji ni jukwaa muhimu la elimu kwa jamii," alisema Bi. Sanga.

Aidha, Bi. Sanga aliwaomba wanakwaya kuptitaa viongozi wao kualika Ofisi ya EWURA CCC Mkoa wa Ruvuma pale wanapokuwa na makongamano yanayoshirikisha kwaya zingine ili EWURA CCC iweze kutumia jukwaa hilo kutoa elimu inayohusu huduma za nishati na maji kwa makundi mengine pia.

Kwa upande wake mmoja wa viongozi wa Kwaya hiyo Bi. Stella Mu-hagama alisema kuwa Kwaya yao inashukuru kwa elimu waliyoipata na kuahidi kufanyia kazi na kuwa mabalozi kwa jamii inayowazunguka.

Bi. Mu-hagama alisema wao wana fursa ya kukutana na makundi mengine ya uimbaji na hivyo kuwa na nafasi nzuri ya kutoa elimu waliyoipata na kuwa mabalozi kwa wengine.

"Tunaahidi kufanyia kazi elimu tulioipata na kila tupatapo nafasi tutasambaza elimu hii na kuhamasisha wanakwaya wengine pamoja na jamii inayotuzunguka hususani suala la haki na wajibu kama watumiaji wa huduma ya nishati na maji kwa kuwa watu wengi bado hawajui haki na wajibu wao kuhusu huduma za nishati na maji," alisema Bi. Mu-hagama.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mko-wa Ruvuma Bw. Edmund Mnyawami aliwahakikisha wanakwaya hao kuwa milango ya Baraza ipo wazi kwa ajili ya kuwahudumia watumiaji wa huduma za nishati na maji pindi wanapata changamoto au kero kutoka kwa watoa huduma.

"Milango ya Baraza iko wazi na liko tayari kuwahudumia watumiaji wa huduma za nishati na maji, ikiwemo kupokea malalamiko yao kuhusu huduma hizo na kuwashauri namna sahihi ya kuyatatuwa, hivyo wasisite kutoa taarifa na kulalamika pindi wanapokutana na changamoto katika huduma hizo," alisema Bw. Mnyawami.

**WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA IRINGA (IRUWASA)**

**“Ndugu mteja hutakiwi kutoa fedha kwa mtu yeyote
akufanyie malipo. Malipo yote IRUWASA yafanyike kuptitaa
namba maalum ya malipo.**

0800 110 122 | @iruwa.sa | @IruwasaIringa

Toeni elimu kwa wateja wenu - EWURA CCC

Na mwandishi wetu, Rukwa

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoani Rukwa imewaasa wasambazaji na wauzaji wa jumla na reja reja wa bidhaa ya gesi ya kupikia majumbani (LPG) kutoa elimu sahihi kwa watumiaji wa huduma hiyo ili kupunguza madhara yanayoweza kusababishwa na matumizi mabaya ya bidhaa hiyo.

Hayo yamesemwa wakati wa mwendelezo wa semina ya kuwajengea uwezo wasambazaji na wauzaji wa gesi mkoani humo ilioandaliiwa na Kampuni ya Gesi ya Oryx ikishirikiana na EWURA CCC pamoja na taasisi zingine lengo likiwa ni kuwakumbusha na kuwapa taarifa mpya zinazohusu bidhaa za gesi, ili kulinda usalama na kuleta unafuu kwa watumiaji.

Awali katika semina hiyo, wasambazaji na wauzaji wa bidhaa hiyo walielimishwa kuhusu usalama wa bidhaa hiyo, ubandikaji wa bei halali katika maduka yao pamoja na kuzingatia uadilifu kwa kuwa na mizani yenye kupima ujazo halisi wa mitungi ya gesi ili kumlinda mtumiaji.

Akieleimisha kuhusu matumizi sahihi ya gesi ya kupikia, Afisa Huduma kwa Wateja EWURA CCC Rukwa, ndugu Ramadhan Kakende, alisema kuwa ni jambo la muhimu kwa wauzaji wa gesi kuhakikisha wanatoa elimu ya matumizi sahihi ya huduma hiyo kwa wateja wao, kuanzia namna ya kusafirisha mitungi ya gesi, kutumia na sehemu sahihi ya kuhifadhi mitungi hiyo.

"Niwaase ndugu zangu kuhakikisha mnatoa elimu ya matumizi sahihi ya huduma hii kwa watumiaji, kwani kila siku watumiaji wapya wa huduma hii wanaongezeka wakiwa hawana elimu juu ya matumizi sahihi ya huduma hii. Endeleeni kuwakumbusha pia hata wale watumiaji wa zamani kuzingatia kanuni za usalama wa huduma hii ikiwemo usafirishaji salama wa mitungi, namna ya kutumia na sehemu sahihi ya kuhifadhi mitungi wa gesi," alisema Bw.

Kakende.

Bw. Kakende aliendelea kusema, "leo hii tuko hapa kwa ajili ya kuwajengea uwezo ninyi wauzaji, vivyo hiyo nanyi mkawajengnee uwezo watumiaji ambao ni wateja wenu ili kulinda usalama wao, lakini pia kuhakikisha muendelezo na kuaminika kwa biashara yenu.

Ni muhimu pia kuwapimia wateja wenu mitungi ya gesi wanaponunu ili kubaini ujazo halisi wa gesi na kuwapatia mitungi isiyo na hitilafu. Pia mitungi inapaswa kusafirishwa ikiwa wima na kuhifadhiwa sehemu yenye hewa ya kutosha na mbali na vyanzo vya moto"

Aidha Bw. Kakende aliuomba uongozi wa Oryx kutengeneza vipeperushi vyenye elimu hii na kuvisambaza kwa wauzaji na wasambazaji wao ambao nao watakuwa na wajibu wa kuwagawia wateja wao pindi wanapokuja kununua Gesi.

Naye, Meneja wa Wakala wa Vipimo mkoani Rukwa Bw. Deogratius Hussein aliwasisitiza wasambazaji na wauzaji wa gesi kuzingatia uuzaaji ulio salama kwa wateja na kuzingatia ujazo sahihi wa gesi kama sheria in-

avyoolekeza.

"Niwaombe wasambazaji na wauzaji wa gesi mzingatie masuala ya usalama wa wateja wenu pia kuzingatia ujazo sahihi wa mitungi mnapowauzia wateja kwa kupima mitungi kabla ya kuuza," alisema Bw. Hussein.

Mwakilishi wa wauzaji wa gesi waliohudhuria semina hiyo Bw. Bruno Chaka alishukuru kwa elimu waliyoipata toka EWURA CCC na taasisi zingine zilizoshiriki semina hiyo kwani elimu hiyo itaenda kuchangia katika usalama wa bidhaa hiyo na muendelezo wa biashara hiyo.

"Binafsi nashukuru kwa elimu hii tulioipata kutoka EWURA CCC na taasisi zingine kwani zinaimarisha usalama wetu na wateja wetu lakini pia kulinda biashara zetu. Niwaombe wfanyakibashara wenzangu tuzingatia kile tulichofundishwa na kukifanya kazi," alisema Bw. Chaka. Bw. Chaka aliahidi na kuwaomba wauzaji na wasambaji wengine kuendelea kutoa elimu hiyo mara kwa mara kwa wateja wao kila wanapouza nishati hiyo ya kupikia.

EWURA CCC imekuwa ikitumia fursa mbalimbali kuwafikia watumiaji wa huduma za nishati na maji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Baraza ikiwemo watoa huduma pamoja na taasisi ya Wakala wa Vipimo.

Maelekezo

Ujue uzito wa mitungi ya gesi unayonunua

Na Chipegwa Samwel, Morogoro

Gesi ya kupikia ni mojawapo ya vyanzo vikuu vya nishati vina-vyotumika majumbani na kwenye maeneo ya biashara nyingi katika nchi yetu.

Waweza kuwa unafahamu, lakini hata hivyo hebu tujikumbushe kidogo juu ya uzito wa gesi unayonunua kwenye mtungi.

Wakati tunanunua mitungi ya gesi wengi wetu hufanya makosa kwa kutohakiki uzito halisi wa gesi iliyomo kwenye mitungi hiyo jambo ambalo linaweza kuathiri matumizi yetu ya kila siku, gharama tunazopata na hata usalama wetu.

Makala hii imejikita kujadili umuhimu wa mnunuzi wa gesi za kupikia kuelewa uzito halisi wa gesi anayonunua kwa kuzingatia yafuatayo:-

Mteja wa gesi ni muhimu attambue maana halisi ya namba zilizoandikwa kwenye mitungi

Namba zilizoandikwa kwenye mitungi ya gesi huonesha uzito wa mtungi mtupu na uzito wa mtungi ukiwa na gesi kwa pamoja. Kanuni za Vipimo (Uuzaji wa Gesi ya Petroli inayouzwa katika Mitungi) ya mwaka 2013 zinaleza:-

■ Kanuni ya 3 inaa giza kuwa uzito wa mtungi tupu, uzito halisi na uzito wa jumla utaandikwa kwa uwazi.

■ Kanuni ya 4 (d, e na f) inasema kuwa taarifa zifuatazo zita-kuwa zimeandikwa kwa usahili na kudumu kuzunguka shingo mtungi wowote wa gesi;
 d. uzito wa mtungi mtupu
 e. uzito halisi
 f. uzito wa jumla

Je ni muhimu kwa wauza gesi wa rejareja kuwa na mizani?

■ Kanuni ya 6 ya Kanuni za Vipimo (Uuzaji wa Gesi ya Petroli inayouzwa katika Mitungi), 2013

inaelekeza kila muuzaji wa gesi za kupikia ikiwemo muuzaji wa rejareja awe na mzani wa kupimia gesi ilioainishwa.

Je uzito ulioandikwa kwenye mtungi, ukipimwa kwenye mzani, utalingana na ujazo halisi wa gesi iliyomo kwenye mtungi?

■ Inawezekana kabisa ukipima uzito kwenye mzani ukalingana na namba za ujazo halisi iliyopo kwenye mtungi au inawezekana usilingane kwa kupungua kidogo. Kanuni ya 7 ya Kanuni za Vipimo (Uuzaji wa Gesi ya Petroli inayouzwa Katika Mitungi) za 2013 inaaelekeza kuwa kiwango kinachoruhusiwa cha utofauti wa ujazo hautakiwi kuzidi asilimia mibili (2%) kwa wauzaji wa rejareja na asilimia moja (asilimia 1) kwa wale wauzaji wakuu.

Ukokotoaji wa uzito uliopungua baada ya kupimwa kwenye mzani;

i. Uzito halali (duka la rejareja)

Mhandisi Hilolimus H. Mahundi, Meneja Wakala wa Vipimo mkoa wa Mwanza anaeleza kuwa ikiwa mtungi wa gesi umeandikwa kuwa na uzito wa jumla ni kilogramu (kg) 30, na mzani unaonesha kilogramu 29.8:-

■ Hatua ya 1: Tafuta utofauti wa uzito ulioandikwa kwenye mtungi utoe uzito uliopatikana baada ya kupima kwenye mzani yaani: kg 30 - kg 29.8 = kg 0.2

■ Hatua ya 2: Tafuta tofauti ya asilimia: $(0.2/30) \times 100 = 0.67\%$ ambayo ni sawa na makadirio ya asilimia 1

■ Upungufu wa asilimia 1 ni ndani ya kiwango kinachoruhusiwa, kwa hiyo uzito uliopimiwa kwenye mtungi huo ni sahihi.

ii. Uzito usio halali/uliopungwa (duka la rejareja)

Mhandisi Mahundi anaeleza

Mizani: Kanuni ya 6 ya Kanuni za Vipimo (Uuzaji wa Gesi ya Petroli inayouzwa katika Mitungi), 2013 inaaelekeza kila muuzaji wa gesi za kupikia ikiwemo muuzaji wa rejareja awe na mzani wa kupimia gesi ilioanishwa.

Ukokotoaji: Tafuta utofauti wa uzito ulioandikwa kwenye mtungi utoe uzito uliopatikana baada ya kupima kwenye mzani yaani:
 $kg 30 - kg 29.8 = kg 0.2$

Haki: Haki ya kuangalia kama mzani una stika ya uthibitisho kutoka Wakala wa Vipimo ili kujiridhisha kwamba mzani huo umethibitishwa kuwa ni sahihi

Wajibu: Wajibu wa kutoa taarifa kwenye ofisi za Wakala wa Vipimo zilizo karibu naye juu ya upungufu wa gesi au kupiga **simu ya bure namba 0800110097** kwa nchi nzima



kuwa ikiwa mtungi wa gesi ume-andikwa kuwa na uzito wa jumla kg 30, na baada ya kupima mzani ukasomeka kg 29:

■ Mchanganuo: Chukua kg 30 - kg 29 = kg 1

■ Tofauti ya asilimia: $(1/30) \times 100 = \text{asilimia } 3.3$

■ Asilimia hii inapita asilimia mbili (2) ya kiwango kinachoruhiwa kisheria, hivyo mteja atakuwa amepunjwa.

Haki na wajibu wa mtumiaji kwenye ununuzi ya gesi zitumika zo majumbani za kwenye mitungi:

Haki

■ Haki ya kununua gesi kwa wauzaji wenyewe mizani

■ Haki ya kuangalia kama mzani una stika ya uthibitisho kutoka Wakala wa Vipimo ili kujiridhisha kwamba mzani huo umethibitishwa kuwa ni sahihi

■ Haki ya kupimiwa mtungi na kujiridhisha na uzito unaotaka kununua

■ Haki ya kuchagua mtungi mwagine mpaka utakapopata mtungi wenyewe uzito unaokubalika kisheria

■ Haki ya kupewa risiti ya manunuzi ya mtungi wa gesi

■ Haki ya kutoa taarifa kwenye ofisi za Wakala wa Vipimo zilizo karibu naye juu ya upungufu wa gesi au kupiga simu ya bure namba 0800110097 kwa nchi nzima

■ Haki ya kuwasilisha lalamiko EWURA CCC au EWURA kwa hatua zaidi.

■ Haki ya kupewa tahadhari kwenye uhifadhi na uzingatiaji wa matumizi sahihi ya gesi

Wajibu

■ Wajibu wa kununua gesi kwa wauzaji wenyewe mizani

■ Wajibu wa kuangalia kama

mzani una stika ya uthibitisho kutoka Wakala wa Vipimo ili kujiridhisha kwamba mzani huo umethibitishwa kuwa ni sahihi

■ Wajibu wa kupima mtungi na kujiridhisha na uzito unaotaka kununua.

■ Wajibu wa kuchagua mtungi mwagine mpaka utakapopata mtungi wenyewe uzito unaokubalika kisheria

■ Wajibu wa kudai risiti ya manunuzi ya mtungi wa gesi

■ Wajibu wa kutoa taarifa kwenye ofisi za Wakala wa Vipimo zilizo karibu naye juu ya upungufu wa gesi au kupiga simu ya bure namba 0800110097 kwa nchi nzima

■ Wajibu wa kuwasilisha lalamiko EWURA CCC au EWURA kwa hatua zaidi.

■ Wajibu wa kuchukua tahadhari kwenye uhifadhi na uzingatiaji wa matumizi sahihi ya gesi.



Bi. Bertha Maqway, Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Tanga, akitoa elimu kwa baadhi ya watumiaji waliotembelea banda la EWURA CCC wakati wa maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani yaliyofanyika kimko katika viwanja vya Shule ya Sekondari Usagarahivi karibuni

Tumieni mafundi wenye leseni - RCC Tanga

Na Nuru Zuberi, Tanga

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya EWURA CCC Tanga, imewaasa wananchi mkoani humo kutumia mafundi wenyewe leseni zinazotolewa na Mamlaka ya Udhhibitii wa Nishati Maji (EWURA) wanapokuwa na uhitaji wa kutandaza mifumo ya umeme kwenye nyumba zao na wajengeta bia ya kukagua mara kwa mara miundombini hiyo, ili kuepuka majanga yanayoweza kutokea kutohana na uchakavu.

Nasaha hiyo imetolewa na Bi. Bertha Maqway, Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Tanga, wakati wa maadhimisho ya kilele cha Siku ya Vijana Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Usagara Jijini humo, am-

bapo Ofisi ya EWURA CCC ilishirki na kutoa elimu kwa wananchi waliohudhuria maadhimisho hayo.

Akitoa elimu kwa wananchi waliotembelea banda la EWURA CCC, Bi Maqway alieleza umuhimu wa kutumia mafundi umeme waliosajiliwa na na kupewa leseni na EWURA, ili kuwa na miundombinu yenye viwanango na usalama.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 19 (1 na 2) cha Kanuni za Umeme na Uungaji Mifumo ya Umeme za mwaaka 2022 tangazo la Serikali Na. 113, mmiliki wa nyumba atatakiwa kutumia fundi mwenye leseni ya EWURA, ili kujenga mifumo ya umeme kwenye nyumba yake," alinukuu Bi Maqway.

Akizungumza baada ya kutembelea banda la EWURA CCC, Bw. Hiza Baraka, mkazi wa Kisosora Tanga, alieleza kuridhika na elimu aliopata.

"Leo ndio nimefahamu kwa mara ya kwanza kwamba umeme unaweza kuvuja kama miundombinu haitakaguliwa kwa muda mrefu. Ninaahidi kuwa balozi wa elimu hii kwa wananchi wenzangu, na kuhimiza matumizi ya mafundi umeme waliosajiliwa na EWURA," alisema Bw. Baraka

Naye ndugu Jumanne Shabani, mkazi wa Tanga Chumbageni, alilishukuru Baraza kwa ushiriki wake kwenye maadhimisho hayo na kuwa ulikuwa na manufaa makubwa kwa wananchi waliotembelea banda hilo kwani walipata kuelimishwa pamoja na mambo mengine, kuhusu huduma za nishati na maji.

"Leo tumejua mambo mengi susan suala la umuhimu wa kutumia mafundi waliosajiliwa katika kutandaza mifumo ya umeme majumbani mwetu, na pia umuhimu wa kukagua miundombinu ya umeme kila baada ya miaka mitano. Wengi wetu tulikuwa hatujui kuwa miundombinu ya umeme huwa inachakaa na hata pengine kuleta hatari ya kuunguliwa na nyumaba au kuvuja kwa umeme," alisema Bw. Shabani.

Kupitia Maadhimisho ya kilele cha siku ya Kimataifa ya Vijana Duniani, EWURA CCC imefanikiwa kuwapatia elimu wadau 576 kuhusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.

Fahamu faida za kutumia mita za maji za malipo ya kabla

Na Brenda Magoma, Iringa

Katika enzi hizi za maendeleo ya sayansi na teknolojia, mamlaka nyingi za maji nchini zinaendelea kuboresha huduma zao kwa kutumia mbinu za kisasa kwa lengo la kuboresha huduma na kuimarisha mapato yao.

Mbinu hii inayokua kwa kasi ni ya matumizi ya mita za maji za malipo ya kabla (prepaid water meters) ambazo zinatoa suluhisho kwa changamoto zinazohusiana na usimamizi na malipo ya huduma za maji.

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya EWURA CCC mkoani Iringa, kwa niaba ya watumiaji wa huduma za nishati na maji mkoani humo, hivi karibuni ilifutilia kwa karibu kwa lengo la kutaka kujua ubora na manufaa ya matumizi ya teknolojia hii mpya ya mita za maji za malipo ya kabla.

Kwa mujibu wa Bw. David Mlyapatali, Msimamizi wa Mita za Maji na Upimaji, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA), anaeleza kuwa, ili kutambua ubora na manufaa ya matumizi ya mita za malipo ya kabla ni vyema kwanza kutambua aina za mita zinazotumika kwa wateja.

Bw. Mlyapatali anaeleza kuwa, zipo aina nyingi za mita za maji za malipo ya kabla lakini katika makala hii itajadili aina mbili maarufu zinazotumiwa na IRUWASA ambazo ni Citytaps na Joy 200.

"Citytaps ni aina mojawapo ya mita ambazo hutengenezwa nchini Ufaransa. Mita hizi hutumia teknolojia ya mawimbi (mnara) kwa mawasiliano lakini sifa nyingine ni kwamba unaponuua maji taarifa zinaingia moja kwa moja kwenye mita, yaani bila kuingiza tokeni," anasema Mlyapatali.

Bw. Mlyapatali anaongeza kuwa "aina hii ya mita ina uwezo wa kutoa taarifa kwa mteja na mto huduma endapo maji yatakuwa yanavuja, kutanza kumbukumbu na kutoa taarifa kwa mamlaka ya maji kila baada ya nusu saa. Mita hii pia ina uwezo wa kutuma ujumbe kuhusu matumizi ya mteja na kutoa taarifa kabla ya masaa mawili maji kuisha".

Anaeleza kuwa aina hii ya mita hutumia betri, ambapo ili betri hii idumu zaidi, ni bora kununua maji kwa kiasi kikubwa kwa mkupuo mmoja kwani maji yanapoisha valvu ya mita hujifunga na kujifungua, hivyo kununua maji kidogo hupelekea betri kuisha haraka.

Aina ya pili ya mita za malipo ya kabla zinazotumika na IRUWASA ni Joy 200. Kwa mujibu wa Bw. Mlyapatali aina hii ya mita hutumia mifumo miwili ya usomaji, yaani analogia na digitali. Mfumo wa digitali ukishindwa basi mfumo wa analogia utaendelea kufanya kazi.

Bw. Mlyapatali anaeleza kuwa, "kama iliyovo kwa Citytaps, Joy 200 pia hutumia betri, na ili betri idumu zaidi ni bora mteja kununua maji kwa kiasi kikubwa, yaani kwa mkupuo mmoja, kwani maji yanapoisha, valvu ya mita hujifunga na kujifungua hivyo husabisha betri kuisha haraka.

Mlyapatali anasema mteja anaponuna maji kwa njia za kielektroniki huletewa tokeni zenye tarakimu 20 ambazo mteja ataingiza kwenye mita hiyo tayari kwa kupata maji.

Pia anasema mita hizi zinahitaji kufungwa kwenye boksi lake la plastiki muda wote ili kuzikinga na uharibifu unaweza kutohana na mwanga wa juu pamoja na mvua ili ziweze kudumu.

Akieleza faida za kutumia mita za malipo ya kabla kwa ujumla wake, Bw. Mlyapatali anasema kuwa mita hizi zinaondoa changamoto ya mteja ku-

katiwa huduma ya maji kwa sababu ya deni, lakini pia zinamsadia mto huduma kupata mapato kwa uhakika na kwa wakati, hivyo kupunguza gharama za uendeshaji.

"Kwa kutumia mita hizi mtumiaji hulipia kiasi fulani cha fedha kabla ya kutumia maji, hivyo kuhakikisha huduma haitatkatwa kwa sababu ya deni. Mita hizi hupima kwa usahihi kiasi cha maji kilichotumika na kutoa taarifa sahihi kwa mtumiaji kuhusu matumizi yake," alisema Mlyapatali.

Anaongeza kuwa "Mita hizi zinaturahisishia ukusanyaji wa mapato na kuiiondolea Mamlaka changamoto za madeni, na kwamba humjulisha mtumiaji kiasi cha maji kilichobaki hivyo kutoa fursa ya kuongeza salio kabla ya maji kuisha."

Mlyapatali anahitimisha kwa kusema kuwa, mita za malipo ya kabla zina uwezo wa kutoa ripoti ya matumizi, ambapo husaidia watumiaji kufutilia matumizi yao na kupanga matumizi ya baadaye kwa ufanisi zaidi.

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Iringa inatoa wito kwa IRUWASA kuhakikisha inawafungia wateja wake kwenye makundi ya mita za malipo ya kabla kwani zina manufaa si tu kwa wateja wao bali pia kwa mto huduma ambapo zinaongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, kupunguza gharama za uendeshaji na kuepuka malalamiko ya wateja kuhusu bili kubwa za maji.



Makala



Bi. Anadorice Komba, Afisa Huduma kwa Wateja EWURA CCC Kagera, akitoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji kwa vijana na wadau mbalimbali walioshiriki Bonanza lililoandaliwa na taasisi ya TDYA na kufanyika kwenye viwanja vya Kaitaba mjini Bukoba.

RCC Kagera yawafunda vijana

Na Anadorice Komba, Kagera

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Kagera imetumia fursa ya Mabonanza ya makundi ya vijana katika kufikisha elimu inayohusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Hatua hiyo imefikiwa hivi karibuni ambapo Kamati hiyo ilishiriki na kutoa elimu kwa vijana walioshiriki bonanza lililoandaliwa na taasisi isiyi ya kiserikali iitwayo Tanzania Diaspora Youth Association (TDYA), ambapo lengo la tukio hilo lilikuwa ni kuwaunganisha vijana na wadau mbalimbali na kuwapatia elimu, huku vijana hao wakipata fursa ya kushiriki katika michezo na shughuli nyingine.

Akizungumza wakati wa bonanza hilo lililofanya Julai, 2024 na kufikia vijana 789, katika uwanja wa Kaitaba Manispaa ya Bukoba, Bw. Edwin Angelo, ambaye ni Mratibu wa TDYA alisema dhununi la bonanza hilo lil-

ikuwa ni kuwaleta vijana pamoja na kushiriki shughuli za kimichezo, kupeana elimu na kujadili fursa za kiuchumi ambazo vijana wanaweza kuzitumia katika kujikwamua kimaisha.

Angelo alisema, "Lengo la kuanadaa bonanza hili ni kuwaleta pamoja vijana na kuwapa nafasi ya kukutana na wadau mbalimbali, ambapo moja ya wadau muhimu tuliowaalika ni EWURA CCC, ambao kuptia ushiriki wao, walitoa elimu kuhusu masuala ya nishati na maji kwa washiriki."

Alisema bonanza hilo lilijumuisha vijana kutoka viji vijiji vinne vikiwemo vya Lukulungu Wilaya ya Missenyi, pamoja na viji vya Kishogo, Kabale na Luija vilivyoko Wilaya ya Bukoba na hivyo basi kupata fursa nzuri kwa taasisi kama EWURA CCC na zingine kuwapatia vijana hao elimu mbalimbali.

Akieleza kuhusu ushiriki wa Baraza na elimu iliyotolewa wakati wa Bonanza hilo, Bw. Angelo alilipongenza Baraza huku akiwa na matumaini kuwa elimu hiyo itawasaidia vijana hao katika shughuli zao za kila siku.

"Tunaipongeza EWURA CCC kwa elimu mliyotoa, na tunaamini elimu hii

itafanya mabadiliko makubwa kwa vijana wetu. Vijana hawa wanajishughulisha na kazi zinazohitaji nishati ya umeme, hivyo kuptia elimu hii kustumia huduma ya umeme kwa ufaniisi, ili kufanikisha miradi yao," alisema Angelo.

Naye Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Kagera, Bw. Eustadi Katunzi, alieza umuhimu wa tukio hilo kwa kusema, "hii ni fursa adhimu kwa sisi kupata kundi la vijana kwa pamoja. Tunaamini kuptia elimu hii, vijana wamejifunza juu ya haki na wajibu wao wanapotumia huduma za nishati na maji, vidokezo muhimu, pia namna ya kuwasilisha malalamiko pindi wanapopata changamoto. Vijana hawa pia watakuwa mabalizi pindi watakaporudi katika maeneo yao wakisambaza elimu kuhusu EWURA CCC na masuala mengine yanayohusu watumiaji."

Katunzi alisema vijana hao wamefundishwa kwa kina kuhusu haki zao za msingi wanapokuwa wanatumia huduma za nishati na maji, na namna nzuri ya kutumia huduma hizo ili kuepuka gharama kubwa zisizo za lazima, hasa kwa wale wanajishughulisha na ufundi seremala na ufgajji wa kisasa.

Kwa upande wake Bw. Mugisha Kasaaju, mmoja wa wajumbe wa Kamati hiyo alisema kuwa, bonanza hilo limekuwa muhimu kwa kamati kwani imeweza kufikia kundi kubwa la vijana kutoka wilaya mbili kwa wakati mmoja, jambo ambalo ni nadra.

"Kamati itaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na TDYA na taasisi zingine zilizopo mkoani Kagera ili kuendelea kulitangaza Baraza na pia kufikia makundi mbalimbali ya watumiaji hasa wale waliopo pembezoni ambao mara nyangi wanakutana na changamoto wanapokuwa wanatumia huduma lakini hawajui wapi waende au namna gani wawasilishe malalamiko yao." Aliongeza Bw. Kasaaju.

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Kagera imejipanga kuendelea kufikia makundi mengine katika ngazi ya jamii ili kuhakikisha elimu hii muhimu kwa jamii inasambaa katika Mkoa wa Kagera na viunga vyake.

Zingatia haya uwapo kwenye kituo cha mafuta

Na Noela Ntiluvakule, Pwani

Katika mazingira ya vituo vya kujaza mafuta, usalama na tahadhari ni jambo muhimu kwa kila mteja, kwani vituo hivyo ni maeneo nyeti ambayo yanaweza kuwa hatari ikiwa tahadhari za msingi hazitizingatiwa.

Kanuni ya 24(a) (iv) ya Kanuni za Mafuta (Uuzaji wa Rejareja Mijini na Vijijini) za mwaka 2020, Tangazo la Serikali Na. 818, inawataka wenye vituo vya kujaza mafuta kuzingatia usalama wa mali na maisha ya watumiaji wa huduma katika vituo vyao.

Ni wajibu kwa mtumiaji wa huduma za nishati kufahamu na kuzitumia Kanuni hizo anapokuwa katika kituo chochote cha kujaza mafuta.

Makala hii inajadali mambo muhimu anayopaswa kuzingatia mtumiaji wa huduma hii anapokuwa kwenye kituo cha kujaza mafuta ili kuhakikisha usalama wake na wa wengine unazingatiwa wakati wa kupata huduma:-

1. Zima injini ya gari: Mara tu unapofika kwenye kituo cha kujaza mafuta, hakikisha unazima injini ya gari lako. Injini inayowaka inaweza kusababisha cheche na kuchochea moto ikiwa karibu na mafuta yanayomwagika au gesi zinazotoka wakati wa kujaza mafuta. Kuzima injini ni hatua muhimu ya kuzuia ajali zisizotarajiwu na kuimarishe usalama wa eneo hilo.

2. Usivute sigara au kuwasha moto: Kanuni ya 39 (1)(b) na (c) ya Kanuni tajwa inawataka watumiaji kutovuta sigara wala kuwasha moto wowote wanapokuwa kwenye kituo cha kujaza mafuta. Kituo cha kujaza mafuta ni eneo lisiloruhusu uvutaji wa sigara au kuwasha moto wa aina yoyote. Hili ni jambo la kipaumbele katika kuhakikisha usalama wa watu na mali zilizopo katika eneo hilo.

Pia ni muhimu vifaa vya kuzimia moto viwekwe sehemu inayonekana na kuvifiki kwa urahisi katika kituo cha kujaza mafuta pindi panapokuwa

na hatari ya mlipuko wa moto.

3. Tumia Simu kwa uangalifu: Pamoja na kuwa simu ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku, lakini kituo cha kujaza mafuta siyo eneo salama kwa matumizi ya simu. Mawimbi ya redio kutoka kwenye simu yanaweza kusababisha cheche ndogo, ambazo zinaweza kuleta hatari kubwa kwenye eneo lililojaa mvuke wa mafuta. Ni busara kuzima simu yako au kuitumia kwa uangalifu mbali na pampu za mafuta kama Kanuni ya 39 (1)(e) inayovelekeza.

4. Zingatia muda wa kujaza mafuta: Muda mzuri wa kujaza mafuta ni wakati wa asubuhi sana au jioni wakati ardhi ikiwa na ubaridi. Matanki ya kuhifadhia mafuta hujengwa chini ya ardhi, hivyo ardhi inapokuwa na ubaridi mafuta huwa mazito na inapopata joto petroli hupanuka na kupotenza ujazo sahihi. Kujaza mafuta asubuhi au jioni sana itakusaidia kupata ujazo kamili na kuepuka kupoteza thamani halisi ya pesa zako.

5. Epuka kujaza mafuta wakati gari la mafuta linamimina mafuta kwenye matanki: Epuka kujaza mafuta kwenye gari wakati gari la mafuta linamimina mafuta kwenye matanki ya kuhifadhia mafuta. Hii inasaidia kuepuka kupata mafuta machafu endapo mafuta yanayowekwa yatajichanganya na mafuta machafu yaliyopo kwenye kina cha tanki lilipo ardhini, jambo amballo linaweza kuleta madhara kwenye

injini yako.

6. Hakiki ubora wa mafuta unayojaza: Ni muhimu kuhakikisha kuwa mafuta unayojaza ni aina sahihi kwa gari lako. Angalia alama za mafuta zinazoonesa aina mbalimbali za mafuta (kama vile petroli, dizeli, au mafuta mengine ya injini) ili kuepuka kujaza mafuta yasiyosahili ambayo yanaweza kuharibu injini ya chombo chako.

7. Dai risiti ya malipo: Hakikisha unadai risiti halali ya malipo inayoundana na kiasi cha fedha ulicholipa kama inavyoonekana katika bango la bei katika kituo husika. Risiti halali ni uthibitisho muhimu wa malipo yako na inasaidia katika kutatta changamoto yoyote inayoweza kutokea kutohana na bidhaa ya mafuta uliyonunua. Risiti inaweza kutumika kama ushahidi pindi mafuta uliyonunua yatakuwa na hitilafu na pengine yakasababisha dosari katika chombo chako cha moto.

8. Heshimu alama na maonyo yoyote: Kituo cha mafuta kina alama mbalimbali za onyo na maelekezo muhimu. Hakikisha unazisoma na kuziheshimu alama hizi kwani zinaweza kukuongoza kuelewa kuhusu maeneo hararishi, taratibu za kiusalama, na huduma zinazopatikana katika kituo husika.

9. Ripoti changamoto au shida zilizopo: Ikiwa unakutana na changamoto yoyote, kama vile kifaa kisichofanya kazi, mafuta yanayomwagika, wizi au usumbu mwingine wowote, toa taarifa kwa mto huduma. Ikiwa tatizo halitatuliwi, toa taarifa EWURA, ili hatua za haraka zichukuliwe pasipo kuchelewa. Watumiaji wa bidhaa za petroli wanaaswa kuchukua tahadhar i zinazohitajika na kuzingatia maelekezo yote ya kiusalama wakati wote wanapokuwa katika vituo vya kujaza mafuta kwa ajili ya usalama wao na vyombo vyao.



HabariPicha



Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Ruvuma
ndugu Ladslaus Bigambo akitoa elimu kuhusu Baraza na Kazi zake kwa
Wananchi wa mtaa wa Mateka Manispaa ya Songea hivi karibuni.



Mantanki yanayomilikiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Geita yanayotumika
katika kusafisha na kutibu maji kabla hayajawafikia watumiaji wa huduma hiyo.



Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Geita
wakitembelea Mradi wa Maji wa Nyankanga, unaosimamiwa na Mamlaka ya
Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita, kujifunza mchakato wa usafirishaji na
utibuaji wa maji kabla ya kuwafikia watumiaji.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TANGA
(TANGA UWASA)



"ISO 9001:2015"



#TANGAUWASA_UPDATES

SEP 3, 2024

TANGA UWASA MTAALI KWA MTAALI KUHAMASISHA MALIPO YA BILI ZA MAJI

© @tangauwasa ☎ 0800110111 Bure ☎ 0735 800 111

Kila Tome Lina thamani



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (TUWASA)



ZOEZI LA KUSITISHA HUDUMA KWA WADAIWA LINAANZA SIKU YA LEO

Zoezi la kudai Madeni ya Nyuma na Bili za Maji
kwa Wadaiwa Wote linaanza Siku ya Leo
Mtaa kwa Mtaa, Lipa Bili yako sasa kabla ya kusitishiwa
Huduma ya Maji na kulipa Faini ya kurejeshewa Huduma.

LIPA BILI KWA NJIA YA SIMU	
	*150*00# Lipa Kwa M-pesa
	*150*60# Lipa Bili
	*150*88# Lipa kwa Halopesa
	*150*71# Lipa Bili
	*150*01# Lipa Bili
LIPA BILI KWA NJIA YA BENKI	

📞 0800780063 Ⓛ tuwasatabora.3 📱 tuwasa_tabora 🌐 www.tuwasa.go.tz

Vijue viwango vya huduma za majisafi na usafi wa mazingira

Na Ramadhan Kakende, Rukwa

Maji ni mionganoni mwa huduma muhimu katika maisha ya mwanadamu na viumbe wengine. Maji pia hutumika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kuanzia ngazi ya mtu binafsi, familia, viwanda au taasisi.

Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira zilizoundwa kisheria chini ya kifungu cha 9 cha Sheria ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira namba 5 ya mwaka 2019 zina wajibu wa kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wakazi wote katika miji miji midogo, mikubwa na majiji.

Katika kuhakikisha mamlaka za maji zinatoa huduma kwa ubora, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imekuwa ikitoa kanuni na miongozo mbalimbali zikiwemo Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira za mwaka 2020.

Sambamba na Kanuni tajwa hapo juu, Kifungu cha 34 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, (EWURA) ya mwaka 2001, kinaipatia EWURA mamlaka ya kushughulikia malalamiko dhi-

di ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira ili kuhakikisha kuwa migogoro itokanayo na huduma hizo inapatiwa utatuza kwa wakati, weledi na ufansi.

Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira za Mwaka 2020 zimetaja pia faini au fidia amba zo mto huduma anaweza kulazimika kulipa endapo atashindwa kukidhi viwango viliwyowekwa.

Ni muhimu kwa watumiaji kufahamu viwango hivi vya huduma viliwyowekwa kisheria ili kuhakikisha wanapata huduma kulingana na viwango hivyo, ikiwemo kuwajibika au kudai haki zao endapo wataona zinakiukwa na watoa huduma.

Makala hii inaangazia viwango vya utoaji huduma za majisafi na usafi wa mazingira zilizowekwa katika Kanuni tajwa hapo juu:-

Muda wa kuunganishwa na huduma: Kwa mujibu wa Kanuni ya 54 (1) (b) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, za mwaka 2020, maunganisho ya huduma ya maji yatafanyika ndani ya siku saba (7) baada ya mteja kukidhi vigezo ikiwemo kufanya malipo yanayotakiwa. Mteja anapocheleweshwa kuunganishiwa huduma anatakiwa kulalamika kwa maandishi na kudai

fidia ya shilingi 15,000 kwa siku ya kwanza ya kucheleweshewa huduma, na shilingi 5,000 kwa kila siku zinazofuata. Viwango hivi vimetajwa katika jedwali la viwango vya ubora wa huduma pamoja na fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango viliwyowekwa katika Kanuni tajwa.

Ikiwa mteja hana uhakika wa nini cha kufanya katika kuwasilisha lalamiko lake, anaweza kufika katika Ofisi za Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) au Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji katika mkoa wake kwa msaada zaidi. Kifungu namba 4 cha Kanuni za EWURA za utatuza wa migogoro za mwaka 2020, kinalipatia mamlaka Baraza kuawakilisha watumiaji au kulalamika kwa niaba yao.

Ukarabati au ubadilishaji wa mita mbovu: Kanuni ya 39 (2)(a&b) inaeleza wajibu wa mteja katika kutoa taarifa kwa mto huduma juu ya uharibifu wowote wa mita utakao-jitokeza na taarifa ikishatolewa kwa mto huduma kuhusu changamoto ya mita ya mteja, lalamiko hilo linat-akiwa kushughulikiwa ndani ya siku 15 baada ya taarifa kutolewa.

Endapo siku 15 zitapita bila mteja kuhudumiwa basi mteja huyo anatakiwa kumlalamikia mto huduma kwa maandishi na kudai fidia ya shilingi za Kitanzania 15,000 kwa siku ya kwanza na shilingi 5,000 kwa kila siku zinazofuata kama ilivyotajwa katika jedwali la fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma katika Kanuni hizo.

Kuletewa ankara (bill) ya maji bila kusoma mita (dira): Kanuni ya 42 (1) katika taja hapo juu, inaeleza kuwa mto huduma lazima asome mita ya mteja wake ili kuju matumizi sahihi ya mtumiaji, na Kanuni ya 42 (2) inaeleza kuwa mto huduma atamkadiria mtumiaji endapo mita yake imeharibika kwa kuzingatia matumizi ya miezi mitatu inayotangulia kabla ya mita kuharibika. Endapo mteja atapokea ankara au bili ya maji bila mita kusomwa au bila kuambiwa ni kwa nini anakadirwa na akaridhika, basi mteja huyo anatakiwa alalamike kwa mto huduma kwa maandishi na kudai fidia ya kuanzia shilingi za Kitanzania 15,000 kwa kila siku ya kwanza na 5,000 kwa kila siku zinazofuata, kama il-



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (TUWASA)

KWA PAMOJA
TUNAWEZA KUZUIA UPOTEVU WA MAJI

Tafadhali Wasilisha Taarifa za Hitilafu ya Miundombinu ya Maji ili kufanyiwa kazi Haraka

Kwa Pamoja Tununze na Kulinda Miundombinu ya Maji.

0800780063 | tuwasatabora.tz | [@tuwasa_tabora](mailto:tuwasa_tabora) | www.tuwasa.go.tz

**MAMLAKA YA MAJISAFI
NA USAFI WA MAZINGIRA
MUSOMA**

KWA WAKALA?

SIO LAZIMA FANYA MALIPO
POPOTE WIKIENDI HII



[muwasamusoma](#)
[PIGA BURE](#)
[WhatsApp Tu](#)

[0800 108 110](#)

[0615 791 939](#)

ivyotajwa katika jedwali la fidia la Kanuni tajwa kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma.

Ukataji wa huduma kimakosa:
Kwa mujibu wa Kanuni ya 57 (3) (c), (d) na (e) ya Kanuni tajwa hapo juu, endapo mteja anadaiwa basi haitakiwi kumkatia huduma ya maji kwa siku za jumamosi na jumapili, siku za mapumziko ya kitaifa au siku za Ijumaa baada ya saa sita mchana.

Endapo mteja atakatiwa huduma ya maji kimakosa basi atatakiwa alalameke na huduma itatakiwa irejeshwe ndani ya masaa 24 tangu huduma ilipositishwa. Ikiwa masaa hayo 24 yatapita bila huduma kurejeshwa basi mteja anapaswa kumlalamikia mtohuduma kwa maandishi na kudai fidia ya shilingi za Kitanzania 100,000 kwa siku ya kwanza na 5,000 kwa kila siku zinazofuata. Viwango hivi vimetajwa katika jedwali la fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma katika Kanuni za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira za mwaka 2020.

Urejeshaji wa huduma iliyokatwa kutokana na deni: Kwa mujibu wa jedwali la fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma katika Kanuni hizo, kama mteja amekatiwa huduma kutokana na deni lake na ikatokea mteja amelipa deni lote na gharama za kurejeshewa huduma basi huduma inatakiwa irejeshwe ndani ya masaa 24.

Endapo yatapita masaa hayo bila huduma kurejeshwa, basi mteja huyo ana haki ya kumlalamikia mtohuduma kwa maandishi na kudai fidia ya shilingi za Kitanzania 30,000 kwa

siku ya kwanza na 5,000 kwa kila siku zinazofuata kama ilivyotajwa katika jedwali hilo la fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma.

Kuchelewa kujibiwa malalamikoyasiyohusu bili au ankara ya maji: Lalamiko lolote lisilohusu bili au ankara ya maji linatakiwa kujibiwa ndani ya siku 5 za kazi ikimaanisha uchunguzi uwe umeshafanyika na kutolewa majibu. Endapo zitapita siku hizo bila majibu, basi mteja atatakiwa kulalamikia tena kwa maandishi na kudai fidia ya shilingi za Kitanzania 30,000 kwa siku ya kwanza na 5,000 kwa kila siku zinazofuata kama ilivyotajwa katika jedwali la fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma katika Kanuni tajwa hapo juu.

Kuchelewa kujibiwa malalamikoyanayohusu ankara ya maji: Kwa mujibu wa jedwali la fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma katika Kanuni hizo, malalamiko yote yanayohusu ankara ya maji yanatakiwa yajibie ndani ya siku 5 za kazi tangu kupokelewa kwa lalamiko hilo, ikimaanisha uchunguzi uwe umeshafanyika na kutolewa majibu.

Endapo zitapita siku hizo bila majibu mteja ana haki na wajibu wa kumlalamikia tena mtohuduma kwa maandishi kwa kuchelewa kujibiwa lalamiko lake na kudai fidia ya shilingi za kitanzania 30,000 kwa siku ya kwanza na 5,000 kwa kila siku zinazofuata kama ilivyotajwa katika jedwali hilo la fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma katika Kanuni tajwa hapo juu.

Kutiririka kwa maji machafu ndani ya nyumba au makazi ya

mteja: Utiririshaji wa maji machafu hautaruhusiwa, na hii ni kutoka katika jedwali la fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma katika Kanuni hizo za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira za mwaka 2020.

Endapo maji machafu toka katika mfumo wa majitaka unaomilikiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira yakatiririka ndani ya nyumba au jengo la mteja basi inatakiwa kushughulikiwa mara moja na Mamlaka husika baada ya taarifa kutolewa. Mteja anatakiwa kutoa taarifa mapema juu ya utiririkaji wa maji hayo kwa Mamlaka husika na akipuuzwa anayo haki ya kudai fidia ya shilingi za Kitanzania 50,000 kwa siku ya kwanza na 20,000 kwa kila siku zinazofuata kama ilivyotajwa katika jedwali hilo la fidia la Kanuni hizo.

Kutiririka kwa maji machafu nje au kwenye shamba au kiwanja cha

mteja: Utiririshaji wa maji machafu hautaruhusiwa ili kulinda afya na usalama wa mtumiaji, na hii ni kutoka katika jedwali la fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma katika Kanuni hizo za Ubora wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira za mwaka 2020

Endapo maji machafu toka katika mfumo wa majitaka unaomilikiwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira yakatiririka kwenye shamba au kiwanja cha mteja basi inatakiwa kushughulikiwa haraka sana na Mamlaka husika baada ya taarifa kutolewa. Mteja anatakiwa kutoa taarifa mapema juu ya utiririkaji wa maji hayo kwa mamlaka husika na akipuuzwa anaweza kudai fidia ya shilingi za Kitanzania 30,000 kwa kila siku ya kwanza na 20,000 kwa kila siku zinazofuata kama ilivyotajwa katika jedwali hilo la fidia kwa kushindwa kufikia malengo au viwango vya huduma katika Kanuni hizo.

Ikiwa mteja hana uhakika wa nini cha kufanya katika kuwasilisha lalamiko lake anaweza kufika katika ofisi za EWURA CCC au Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji katika mkoaa wake kwa msaada zaidi.

EWURA CCC inapenda kuwaasa watoa huduma na watumiaji kuzingatia viwango hivi kwani ndio msingi wa huduma bora ya maji na vikipuuzwa huongeza malalmiko na migogoro katika huduma hizi na hatimaye wanachi huweza kuondoa imani kwa watoa huduma na serikali kwa ujumla.

Uwajibikaji

Usiruhusu upopo ukupige, linda bajeti yako ya maji

Na Sakina Yusuf, Tabora.

Je, umewahi kuijuliza kwa nini bili yako ya maji inaongezeka ghafla licha ya kutoongeza matumizi yako? au labda umewahi kuona mita yako ya maji ikizunguka wakati maji yamekatika? Ikiwa ndivyo, huenda unakabiliwa na tatizo la upopo kwenye mabomba yako.

Upopo unaopita kwenye mabomba yako ya maji na hatimaye kwenye mita unawenza kusababisha ongezeko la bili ya maji na hata uharibifu wa miundombinu yako ya maji.

Makala hii inaangazia sababu za uwepo wa upopo kwenye mabomba, athari zake na namna ya kuzuia au kutatua tatizo hili.

Zipo sababu zinazosababisha upopo kuingia ndani ya mabomba wakati wa usambazaji maji kama zinavyoelezwa na Afisa Mfumo Taarifa za Kijiografia kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabo-ra (TUWASA), Bw. Meleka Wanzalaki ambaye anaeleza baadhi ya sababu hizo na namna ya kudhibiti kama ifuatavyo:-

1. Mfumo wa mabomba kutokufungwa vizuri na kusababisha upopo kuingia ndani ya mabomba ya maji;

2. Bomba likipasuka na kufanya sehemu iliyopasuka kuruhusu upopo kuingia ndani ya mabomba;

3. Kuacha wazi kwa mabomba wakati wa matengenezo na hivyo kuruhusu upopo kuingia kwenye mfumo wa mabomba husika; na

4. Upopo kuingia wakati wa kusukuma maji kutoka kwenye chanzo cha maji na kujaa kwenye mabomba.

Upopo ukiwa mwangi kwenye mabomba nini hutoka?

1. Kama msukumo wa maji (pressure) ni mdogo hali hii huchangia wateja kukosa maji, maana upopo mwangi huwa ni kizingiti kuzuia maji kwenda kwa mteja kwa nafasi;

2. Upopo unawenza kuchangia bili za maji kuwa kubwa ikiwa hau-tadhibitiwa kwani utasababisha mita ya maji kutembea na kusoma matumizi ya maji wakati maji hayatoki.

Nini hufanyika kuzuia upopo ku-

jaa kwenye mabomba makubwa kwa upande wa TUWASA

Bw. Wanzalaki anaeleza kuwa kwenye mtandao wa mabomba makubwa ya maji, TUWASA ime-funga Vali za hewa (Air Valve) kila sehemu kutoka kwenye chanzo hadi kwa wateja ili kuruhusu upopo kutoka kabla haujapita kwenye mita za wateja.

Kwa upande wa mtumiaji, ni muhimu kufanya yafuatayo ili kudhibiti bili kubwa zinazosababishwa na upopo kuingia kwenye mita:

Funga mabomba yako

Bw. Wanzalaki anaeleza kuwa watumiaji wa huduma ya maji wanatakiwa kuhakikisha wanafunga mabomba yao vizuri wanapokuwa hawatumii maji kwa muda mrefu, au kipindi cha uhaba wa maji ili kupunguza nafasi ya upopo kuingia kwenye mfumo wako wa maji. Kuacha wazi mabomba kutasababisha upopo kupita kipindi huduma ya maji inaporejea. Maji yanapoanza kusambazwa kwenye mabomba, upopo uliokuwepo kwenye mabomba hayo hutafuta sehemu ya kutokea na hivyo ikiwa bomba litakuwa wazi upopo utapata nafasi ya kupita na kufanya mita yako kutembea na kuongeza bili.

Tumia mafundi wenye sifa kukagua miundombinu ya maji

Bw. Wanzalaki anawasisitiza watumiaji wa huduma ya maji kujenga tabia ya kukagua mara kwa mara



miundombinu ya maji kwa kutumia mafundi wenye sifa stahiki. Watalaamu hawa wanawenza kugundua mipasuko na kurekebisha matatizo yoyote yanayoweza kusababisha upopo kuingia kwenye mabomba ya mteja.

Tumia vifaa imara katika uwekaji wa miundombinu ya maji

Inashauriwa kutumia vifaa vyenye ubora wa juu vinavyowenza kuhimili kuzuia upopo kuingia kwenye mabomba. Wateja watumie vifaa imara na vya kisasa wakati wa kuweka au kuboresha miundombinu yako ya maji.

Kagua mita yako ya maji mara kwa mara

Wanzalaki anashauri pia watumiaji wa huduma ya maji kakagua mita zao za maji mara kwa mara ili kujiridhisha kama zinafanya kazi vizuri, na ikiwa mita yako inaonesha matumizi yasiyo ya kawaida basi inaweza kuwa ni ishara ya hitilafu ya upopo kuingia kwenye mfumo wako wa maji.

Acha vali ya mlango (Gate Valve) yako wazi

Akihitimisha, Bw. Wanzalaki anasilitiza watumiaji wa huduma ya maji kuhakikisha muda wote vali za mlango za mita zao kuwa wazi ili kuruhusu uwepo wa maji kwenye mabomba na hivyo kuепusha upopo kukaa na ikitokea huduma ya maji imerejea na mteja akaona kuna upopo na mgandamizo (pressure) kubwa basi afunge bomba na asubiri kwa dakika kadhaa ili kupisha upopo.

Kwa wateja wa TUWASA, Bw. Wanzalaki alieleza kuwa Mamlaka hiyo ina mipango endelevu ya kuongeza vali za mlango katika mabomba makubwa yanayopitisha maji ili kupunguza uwepo wa upopo kwenye mabomba ya wateja.

EWURA CCC itaendelea kutoa elimu kuhusu masuala mbalimbali yanayomhusu mtumiaji wa huduma za nishati na maji ikiwemo suala la kudhibiti ongezeko la bili zinazowenza kusababishwa na upopo kwenye mita za maji.

Tusemeeni - Wazee

Na Geoffrey Sokesia, Singida

Wazee na watu wasioji-weza mkoani Singida wameliom Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kupaza sauti kwa nibaba yao ili Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA) iwapatie msamaha wa huduma ya maji kutokana na kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama hizo.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na baadhi ya wazee wakazi wa Mtaa wa Mnung'una Manispaa ya Singida, wakati wa mukutano wa wananchi wa Mtaa huo, ambapo Ofisi ya EWURA CCC Mkoa wa Singida ilialikwa ili kutoa elimu kuhusu huduma za nishati na maji.

Akiongea katika mukutano huo Bw. Juma Kangani alisema kuwa, katika mtaa wao kuna baadhi ya wazee na watu wenyewe mahitaji maalumu ambaeo upata huduma ya maji kwa shida sana kutokana na kushindwa kumudu gharama za huduma hiyo.

"Baadhi yetu sisi wazee kwa sasa hatuna vipato na hatuna watoto wa kutusaidia kulipia gharama ya maji, hivyo ni muhimu Serikali kuititia Mamlaka ya Maji itutazame kwa jicho la huruma, kwani ni vigumu kuendesha maisha bila uwepo wa maji," alisema Kangani.

Aliomba EWURA CCC kuwase-me a wazee hao kwenye mamlaka za juu na hasa kwa uongozi wa SUWASA, ili kupata msamaha na kupewa bure ndoo kadhaa za maji kwa siku kwenye vioski vinavyomilikiwa na mamlaka hiyo.

Kwa upande wake Bw. Mrisho Mjinga, ambaye pia ni mkazi wa Mtaa huo alisema kuwa, katika jamii yao kuna baadhi ya kaya ambazo ni duni sana kiasi kwamba hazina hata uwezo wa kumudu gharama ya kupata huduma za msingi kama vile maji, hivyo aliomba EWURA CCC kuwatetea wananchi hao ili waweze kupata huduma ya lazima katika Maisha ya kila siku.

"Kaya hizi zipo chache sana kwenye jamii yetu, hivyo naamini Serikali kuititia SUWASA, inaweza ikatafuta utaratibu wa kuwapatia

“
**sisi tumepokea
ombi lenu** na
tutalifikisha katika
ofisi za SUWASA
kwani wao ndio
watoa huduma,
naamini kwa vile
sheria na miongozo
inawaruhusu basi
wanaweze wakawa
na jibu zuri

hawa wenzenetu huduma ya maji bure kwa idadi fulani ya ndoo bila kuaathri mapato ya Mamlaka ya Maji," alisema Mjingga.

Mjingga aliendelea kusema kuwa, anaamini EWURA CCC inaweza ika-wa sauti ya wanajamii hao wachache ambaeo vilio vyao havisikiki, hivyo kuiomba kufikisha hoja hiyo sehemu husika, ili wanajamii wenzao ambaeo hawamudu kabisa gharama za maji nao waweze kupata huduma hiyo.

Akitolea ufanuzi kuhusu ombi la wazee na watu wasiojiweza la kupatiwa msamaha wa huduma ya maji, Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Singida Bi. Everista Lucas alisema kuwa Ofisi ya EWURA CCC imeipokea hoja hiyo na kuahidi kuiflikisha katika ofisi za SUWASA na kuona namna gani sheria inawaruhusu kufanya hivyo.

Alisema kuwa Sheria ya Maji namba 5 ya Mwaka 2019 kifungu cha 23(1) kinaeleza kuwa katika utekelezaji wa madaraka na utekelezaji wa majukumu chini ya kifungu cha 21 (a-c), mamlaka ya maji itazingatia uwepo wa mahitaji ya watu walioko katika hali duni ya kiuchumi wakati wa kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira kwa watu hawa, kuweka viwango na ada nyininge za huduma za maji na usafi wa mazingira na kuchukua hatua yoyote katika masuala ambayo yanaweza kuwa na athari mbaya kwa ustawi wa kiuchumi wa makundi hayo.

Kifungu 23 (2) kinaeleza kuwa

mamlaka ya maji kwa kushirikiana na mamlaka ya Serikali za Mitaa itatambua watu walioko katika hali duni ya kiuchumi.

"Sisi tumepokea ombi lenu na tutalifikisha katika ofisi za SUWASA kwani wao ndio watoa huduma, naamini kwa vile sheria na miongozo inawaruhusu basi wanaweze wakawa na jibu zuri kwenu," alisema Bi. Evarista.

Akizungumza baada ya EWURA CCC kufikisha ofisini kwake hoja juu ya namna gani SUWASA hutoa msamaha wa gharama za maji kwa watu wenye uchumi duni, Mkurugenzi wa Huduma Kwa Wateja Bw. Hossea Magimbi alitoa ufanuzu kuwa, SUWASA kikanuni inawajibika kutoa huduma ya maji bure kwa kaya ambazo hazina uwezo kabisa wa kulipia gharama za huduma ya maji.

Alisema hapo awali utaratibu ulikuwa kwamba, kaya ambazo hazimudu kabisa gharama ya kulipia huduma ya maji zilikuwa zinapewa lita 40 bure kwa siku lakini utaratibu wa sasa kaya hizi zinatakiwa kupewa lita 100 ambayo ni sawa na ndoo 5 za lita ishirini kwa siku.

"Hivi karibuni tulipokea ombi kutoka kwa mwananchi mmoja ambaye alikuwa akiomba msamaha wa gharama za huduma ya maji, nasi tulimuelekeza taratibu za kufuata, ikiwemo kuandika barua ya maombi ambayo itapita kwa Afisa Ustawi wa Jamii, Manispaa ya Singida kwani Afisa Ustawi wa Jamii ndiye mwenye mamlaka ya kuthibitisha kuwa mwananchi huyo ana hali duni kiasi cha kustahili kupatiwa msamaha ndipo nasi tuweze kulifanyia kazi ombi lake." Alisema Magimbi

Magimbi alisema kuwa, utaratibu wa kubaini kaya ambazo zinaiangia kwenye msamaha huo unafanywa na ofisi ya Afisa Ustawi wa Jamii ngazi ya manispaa, kwani yeze ndiye mwenye mamlaka ya kujiridhisha kuwa kaya fulani inatakiwa kupata msamaha huo.

Katika programu zake za uelimishaji, EWURA CCC itaendelea kutoa elimu na kuwajengea uwezo makundi mbalimbali ili kufahamu taratibu zinazopaswa kufuatwa na watumiaji ili kupata haki za msingi.

Uwakiishi

HabariPicha



Mwenyekiti wa Baraza, Mhandisi David Ngula, akimshukuru Mwenyekiti wa Bodii ya Tanga UWASA, Dkt. Fungo A. Fungo, wakati wa ziara ya Baraza kwa Mamlaka hiyo. Ziara hiyo ililenga kuliwezesha Baraza kujifunza namna Tanga UWASA inatao huduma zake na mikakati yake ya uboreshaji wa huduma za maji kupitia uuzaji wa Hatifungani ya Kijani. Ziara hiyo ilifanyika Septemba 2024.



Mha. wa Uzalishaji Maji wa DUWASA Bw. Emmanuel Lugembe, akitoa maelezo kwa Wajumbe wa Baraza walipotembelea kituo cha kusukuma maji cha Mzakwe, kilichopo nje kidogo ya Jiji la Dodoma, ili kujionea jinsi kituo hicho kinavyofanya kazi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tanga UWASA, Mha. Godfrey Hilly, akiwaonesha Wajumbe wa Baraza na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Tanga transforma mpya iliyopo katika Kituo cha Kusambazia Maji cha Mowe. Transforma hiyo inatarajiwa kuboresha upatikanaji wa umeme na huduma za usambazaji maji mkoani humo.



Dkt. James Peter Mataragio, Naibu Katibu Mkuu (Petroli na Gesi), Wizara ya Nishati (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Baraza walipotembelea ofisi ndogo za Wizara hiyo zilizopo Kikuyu, Jijini Dodoma, mapema Novemba 2024, kwa ajili ya ziara ya heshima. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa Baraza Mha. David Ngula na wengine ni Wajumbe wa Baraza, Maafisa wa Wizara na Sekretariat ya EWURA CCC.



Mha. Kenneth Masuki, Makamu Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Itracom Fertilizers Limited kilichopo Dodoma (wa pili kulia), akitoa maelezo kwa Wajumbe wa Baraza, walipotembelea kiwandani hapo kujua mahitaji ya nishati na maji kwa watumiaji wakubwa wa huduma hizo pamoja na kujifunza namna kiwanda hicho kinavyofanya kazi.



Bi. Sakina Yusuf, Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC Tabora, akitoa elimu kuhusu haki na wajibu za watumiaji wa huduma za nishati na maji kwa wafanyakiasa wa Soko la Isevyia (hawako kwenye picha) lililopo katika Manispaa ya Tabora, hivi karibuni.

TUNZA RIMOTI YA MITA YAKO

Uendelee kufurahia huduma



 Ndugu wateja Tunawakumbusha kutunza rimoti za mita za umeme (Customer Interface Unit) ili kuepuka gharama za zida na usumbu wa huduma zitakapoharibika. Gharama za kubadilishiwa rimoti ni shilingi 80,000/= kwa njia moja na 120,000/= kwa njia tatu.

Jinsi ya Kutunza Rimoti

- Toa betri mara baada ya kuingiza umerme ili kuepuka uvujaji.
- Weka rimoti sehemu isiyokuwa na maji au unyevunyevu.
- Weka rimoti sehemu salama isiyoweza kuanguka.
- Toa rimoti kwene umeme baada ya kuingiza umerme.
- Hifadhi rimoti mahali salama ili kuepuka kuchezewa na watoto.



Shiriki kuzuia upotevu wa maji na uharibifu wa miundombinu ya maji

Kwa kupiga Simu Bure:

 **0800 110010**
0677091360





Ni jukumu letu sote kuhakikisha tunalinda miundombinu ya maji

 Piga simu Bure
0800 110010/0677091360

"SOUWASA huduma bora kwa wote"

Baraza lapaza sauti ubovu dira za maji Manyara

Na Neema Nnko, Manyara

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kuititia Kamati yake mkoani Manyara imepaza sauti kwa niaba ya wakazi wa kijiji cha Gichameda-Magugu mkoani humo hivi karibuni baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wakazi wa Kijiji hicho juu ya ubovu wa mita za maji.

Mita hizo zimekuwa zikisababisha wananchi hao kukosa huduma ya maji na hata kusababisha ongezezo la bili zao za maji tofauti na matumizi yao halisi

Baraza lilipokea kero hiyo hivi karibuni wakati Kamati yake mkoani Manyara ilipokuwa ikitoa elimu kwa wananchi wa kijiji hicho kuititia mkutano ulioandaliwa na Serikali ya Kijiji hicho ambapo, wananchi hao walipata fursa ya kueleza kero ya ubovu wa mita hizo.

Akielezea hali hiyo, Bw. Lazaro Laurent ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Gichameda alisema kuwa, amekuwa akipokea malalamiko mengi ya wananchi wake kuhusu ubovu wa dira za maji zinazosababi-

sha wananchi wake wakose huduma ya maji majumbani mwao, lakini pia wakati mwagine mita hizo kusoma uniti nyingi na kusababisha bili kubwa za maji.

Mwenyekiti huyo alieleza kuwa yeye hana utaalamu wa masuala ya mita za maji, hivyo amekuwa akilitolea taarifa suala hilo kwa Mamlaka ya Maji Ofisi ya Magugu na baadaye kutafuta ushauri kwa Mjumbe kutoka Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Manyara kwa msaada zaidi wa ufuatilaji ili kupata suluhisho la changamoto hiyo.

"Nimekuwa nikitoa taarifa kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA) Ofisi ya Magugu ili watatue changamoto ya ubovu wa mita lakini hakuna hatua zozote zilizochukuliwa. Niliongea pia na Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji ya EWURA CCC Mkoa wa Manyara Bw. Deogratius Gallus, kwa msaada zaidi wa ufuatilaji kwa kuwa mimi si mtalalamu wa shughuli hizo," alieleza Bw. Laurent.

Naye Bw. Juma Rajabu Selemani, mkazi wa eneo hilo alieleza kuhusu ubovu wa mita yake ambayo imekuwa ikimsumbuwa kwa muda mrefu, na kwa sasa hana huduma ya maji kabisa

nyumbani kwake.

"Ni miezi miwili toka mita yan-
gu imeharibika, nimetoa taarifa
kwa BAWASA Magugu, lakini bado
hawajatatu changamoto hiyo.
Na mbaya zaidi, sina huduma ya
maji nyumbani kwangu hadi sasa.
Ninateseka kutafuta maji sehemu
nyingine, hivyo tunaomba msaada
ili changamoto hii itatuliwe," alise-
ma Bw. Selemani.

Akifanua kuhusu malalamiko
ya wananchi hao ofisini kwake,
Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka
ya Maji Babati (BAWASA) Mha. Idd
Msuya alikiri kupokea malalamiko
kuhusu ubovu wa mita za maji, na
kuahidi kuwa Mamlaka anajipan-
ga kuja na mkakati wa kubadilisha
mtandao mzima wa maji katika kiji-
ji hicho, ikiwa ni pamoja na mita za
maji ili kuondokana na changamoto
hiyo.

"Nafahamu kuna changamoto
hiyo katika eneo la Gichameda na
sehemu nyingine, lakini nimetenga
kiasi cha shilingi milioni mia moja
kwa ajili ya kubadilisha mtandao
mzima wa maji na mita ambazo
zina changamoto ili kuondokana na
hali hii ya wateja kukosa huduma ya
maji kwa nyakati mbalimbali, kazi
hii itanza muda siyo mrefu," aliele-
za Mha. Msuya

EWURA CCC inaendelea ku-
futilia utatuzi wa changamoto za
watumiaji hao ambapo hadi sasa
utekelezaji wake umefanyika kwa
asilimia 80.

EWURA CCC ANTI-CORRUPTION POLICY

Sera

1. Policy Purpose

The purpose of this policy is to promote ethical conduct and prevent corruption within EWURA CCC. The policy establishes a framework for ensuring that all employees, Councilors, and stakeholders adhere to the highest standards of integrity and transparency in all operations and interactions.

2. Scope

This policy applies to all EWURA CCC Council members, employees, Regional Consumer Committee members, consultants, and any other individuals acting on behalf of the Council. It covers all aspects of EWURA CCC's operations, including financial management, procurement, decision-making, and interactions with external stakeholders.

3. Definition of Corruption

Corruption is defined as the abuse of power for personal gain, or the offering, giving, receiving, or soliciting of anything of value to influence the actions of an official in the discharge of their duties. This includes, but is not limited to:

- Bribery
- Deception
- Intimidation
- Conflict of interest
- Embezzlement
- Any other unethical or illegal activity that undermines transparency and accountability

4. Commitment to Anti-Corruption

EWURA CCC is committed to:

- Zero tolerance for corruption, bribery, or any form of unethical behaviour.
- Conducting its business in an open, fair, and accountable manner.
- Complying with all national and international anti-corruption laws and regulations.
- Promoting a culture of integrity, honesty, and ethical conduct within the Council.

5. Responsibilities

All EWURA CCC Councilors, employees, and RCCs are responsible for:

- Upholding the principles of this policy in all their

actions.

- Reporting any suspected corrupt activities or unethical behaviour.
- Ensuring that their conduct is free from any conflict of interest or personal gain that compromises the integrity of EWURA CCC

6. Reporting and Whistleblowing

EWURA CCC encourages the reporting of any suspected corruption or unethical behaviour through established reporting channels, including:

- Anonymous reporting mechanisms (e.g., hotlines, and suggestion boxes installed at the regional offices)
- Reporting to supervisors.

The identity of whistleblowers will be protected, and EWURA CCC commits to taking appropriate action to investigate reports while ensuring confidentiality and protection against retaliation.

7. Consequences of Violation

Any Council Member, employee, RCC member, or stakeholder found to have engaged in corrupt activities will face disciplinary action, which may include termination, legal prosecution, and any other actions deemed necessary in accordance with national laws and EWURA CCC's internal regulations.

8. Prevention and Awareness

EWURA CCC will:

- Provide regular training and awareness programs on anti-corruption for Council Members and employees.
- Ensure that all stakeholders are aware of the policy and their responsibilities.
- Continuously monitor and assess risks related to corruption within the Council and take appropriate preventive measures.

9. Policy Review

This policy will be reviewed regularly and updated as necessary to ensure it remains effective and aligned with national and international anti-corruption standards.

10. Effective Date

The Policy was effected for implementation by the Council on 30th January 2025.

HabariPicha



Bw. Aloys Alex Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Pwani akitoa elimu juu ya haki na wajibu wa mtumiaji wa huduma za nishati na maji kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Picha ya Ndege iliyopo Kibaha, Mkoani Pwani hivi karibuni.



Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Singida Ndugu Yahaya Seif akitoa maelezo kwa baadhi ya wananchi walitembelea Banda la EWURA CCC wakati wa Maonesho ya Saba ya Mifuko na Programu za Uwezesaji Wananchi Kiuchumi, yaliyofanyika tarehe Septemba 2024 katika viwanja vya Bombadia Manispaa ya Singida.



Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC Tanga Bi. Nuru Zuberi, akisikiliza kero za baadhi ya wananchi wa Kata ya Tangasisi baada ya kutoa elimu kuhusu kazi za Baraza katika viwanja vya Shule ya Msingi Mwakidila tarehe hivi karibuni.

GEUWASA yashauriwa kuongeza upatikanaji maji

Na Wadi Omary, Geita

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya EWURA CCC Geita, imeishauri Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita (GEUWASA) kuongeza kasi ya uzalishaji maji ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Ushauri huo umetolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Bw. Dotto Paul hivi karibuni, kufuatia ziara iliyofanywa na Kamati hiyo kwenye vyanzo vya maji vya GEUWASA.

Akiongea wakati wa ziara hiyo, Bw. Paul alisema kuwa, ziara hiyo ilisukumwa na uwepo wa malalamiko kuhusu upatikanaji wa huduma ya maji kutoka mionganoni mwa wakazi mjini Geita.

"Siku za hivi karibuni tumepokea malalamiko kadhaa kutoka kwa wakazi mbalimbali mjini Geita kuhusu upatikanaji wa maji na hivyo tumeona ni vyema kufanya ziara hii ya kutembelea vyanzo vya uzalishaji maji," alisema

Bw. Paul.

Alieleza kuwa ziara hiyo itaipatia Kamati uelewa wa hali halisi ya upatikanaji wa maji na hatimaye kutoa mrejesho na taarifa sahihi kwa watumiaji ikiwa ni moja ya jukumu la Baraza la kusambaza taarifa zenye maslahi kwa watumiaji.

GEUWASA ilikiri uwepo wa changamoto hiyo ya upatikanaji wa maji na kufanua kuhusu malalamiko hayo kuititia kwa Mhandisi Ernest Enyasi, ambaye ni Msimamizi wa Mtando wa Maji kutoka GEUWASA.

"Kwa miezi mitatu sasa tumekuwa tukipata changamoto ya wateja wetu kuhusu huduma ya maji na hii inasababishwa na uzalishaji wetu kuwa chini kwa kuwa mpaka sasa tunazalisha lita milioni 15 tu kwa siku wakati uhitaji wa maji kwa Geita ni zaidi ya lita milioni 25. Changamoto nyingine ni kupasuka kwa mabomba ya maji hususani katika mitaa ya Kalangalala, Nyakumbu, Buhalala, Bulela na Bombambilii;" alisema Mha. Enyasi.

Ushauri

Alieleza mpango wa Mamlaka hiyo katika kutatua changamoto hiyo kuwa ni kurekebisha na kubadili miundombinu iliyochakaa na kuweka mipyga.

"Kwa sasa tupo kwenye ukarabati wa miundombinu ya maji na tunategemea kumaliza zoezi ili mapema kwa kuondoa mabomba yaliyochakaa na kuweka mabomba mapya," alisema Mha. Enyasi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa GEUWASA, Mhandisi Frank Changawa aliwaeleza Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa, Mamlaka yake imeandaa mpango madhubuti ya muda mfupi na muda mrefu ili kuhakikisha mradji ya kuongeza maji inayoenlelea kutekelezwa inakamilika kwa wakati uliopangwa na hivyo kupunguza changamoto hiyo upungufu huo maji.

Alisema kuwa "mpango wa muda mfupi unahusisha kuongeza chujio la Nyamkanga ambapo uzalishaji utaongezeka kutoka lita milioni 2 hadi lita milioni 5 kwa saa, na pia juhudu kubwa ya kudhibiti maji yanayopotea inafanyakika kwa kupanga mafundi kila mtaa kuhakikisha kwamba bomba linapopasuka fundi husika anafika eneo hilo kwa haraka mara baada ya taarifa kutfukia."

Mhandisi Changawa alisema kuwa katika mpango wa muda mrefu, GEUWASA imepata mradji mkubwa wa maji kutoka Ziwa Viktoria, ujulikanao kama "Mradi wa Miji Ishirini na Nane" ambao unategemewa kukamilika mwezi Desemba 2025 na kuondoa uhaba wa maji katika Kata 13 za Kalangalala, Nyakumbu, Buhalala, Bulela, Bombambilii, Nyanguku, Mtakuja, Bumwang'oko, Kasamwa, Kanyala, Mgusu, Ihanamilo na Shiloleli.

Alisema "hadi sasa matanki mawili yanajengwa ambapo tanki moja la lita elfu tano linajengwa maeneo ya 'Mkoani' na tanki la lita elfu mbili linajengwa maeneo ya 'Mpomvu' kuititia Mradi huo wa Miji Ishirini na Nane kutoka eneo la Senga hadi kufika Geita."

Kwa mujibu wa kifungu namba 30 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, EWURA CCC imepewa majukumu, ikiwemo kuwakilisha watumiaji wa huduma za nishati na maji na kusambaza taarifa muhimu kwa watumiaji hao, pamoja na hali ya upatikanji wa huduma hizo.



Mhandisi Ernest Ghumbi kutoka Kitengo cha Usambazaji Maji na Miundombinu GEUWASA, akieleza namna dira za maji zinavyofanya kazi, wakati wa ziara ya Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Geita walipotembelea chanzo cha maji Nyamkanga.

Mamia waelimishwa soko la Rwanishenye na Kashai

Na Anadorice Komba, Kagera

Kamati ya Watumiaji wa huduma za Nishati na Maji ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Kagera, imewafikia zaidi ya wadau 420 kuitia programu yake mahususi ya elimu masokoni inayolenga kuwafuata watumiaji maeneo walijopo na kuwaelimisha kuhusu masuala ya nishati na maji ili kuwa na mchango katika kuboresha huduma hii nchini.

Kuitia programu hiyo, wadau hao wameelishwa kuhusu haki na wajibu wa mtumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na Malaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati Maji (EWURA), matumizi sahihi na endelevu ya huduma hizo pamoja na utaratibu wa kuwasilisha na kushughulikia malalamiko.

Bw. Oscarion Frances, mkazi wa Mtaa wa Kyamiosi, Manispaa ya

Bukoba ni mmoja wa wanufaika wa elimu hiyo aliyetembelea banda la Kamati na kukiri kuwa na lalamiko la muda mrefu dhidi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), na anaamini baada ya elimu hiyo atachukua hatua stahiki za utatuza wa lalamiko lake.

"TANESCO Bukoba imepitisha nyaya katika kiwanja changi. Nilandika barua kuomba nyaya hizo ziondolewe tangu mwezi Machi 2023, lakini toka wakati huo lalamiko langu halijatatuliwa. Kuitia elimu hii sasa nimeshajua hatua stahiki za kuchukua," alisema Bw. Frances.

Naye Bi. Sada Dauda Mfanya-biashara Soko la Kashai alisema kuwa yeye ana changamoto ya majina ya usajili katika mita ya umeme toka mwaka 2023 na utatuza haujapatikana.

"Nimetoa taarifa TANESCO juu ya changamoto hii lakini bado majina hayajabadilishwa. Kuitia elimu hii nitachukua hatua stahiki kuhu-

su lalamiko langu kwa kuandika barua kwa Meneja wa TANESCO, na kama sitardhishwa basi nitawasilisha lalamiko hili EWURA kwa utatuza zaidi kama tulivyofundishwa," alisema Bi. Dauda.

Akieleza kuhusu programu hiyo ya uelimishaji Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Kagera Bw. Mugisha Kasaaju alisema "programu hii imekuwa na mafanikio makubwa toka tulipolianza. Tumefanikiwa kufikia zaidi ya watumiaji 426 na malalamiko 47 yamepokelewa, 22 ya maji, 22 ya umeme, 01 ya gesi ya kupikia majumbani (LPG) na 02 mafuta, ambayo tumeyafikisha kwa watoa huduma kwa ajili ya utatuza."

Kamati ya Mkoa ya EWURA CCC itaendelea na programu za uelimishaji katika masoko mengine ili kuwajengea watumiaji uwezo wa kujifahamu zaidi Baraza na kazi zake, kufahamu haki na wajibu wao, na elimu kuhusu masuala mtambuka katika sekta za nishati na maji.



Ndugu Mugisha Kaasaju (mwenye koti), Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Kagera akitoa elimu kuhusu kazi za Baraza kwa wajasiriamali katika soko la Rwanishenye mjini humo hivi karibuni.

WIZARA YA MAJI
MAMLUKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA IRINGA (IRUWASA)

Jinsi ya Kupata Deni Lako LA Maji

- Piga *152*00#
- Chagua na.6 maji
- Chagua na.1 huduma za maji za pamoja
- Chagua na.3 uliza deni lako
- Andika akaunti namba
- Unaweza fanya malipo kwa kuchagua lipia

Lipa sasa:

0800 110 122 | @iruwa.sa | @Iruwasa Iringa

Waaswa kushirikiana na kuwajibika

Na Brenda Magoma, Morogoro

Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), Mha. David Ngula, amesitisiza umuhimu wa ushirikiano, weledi na uwajibikaji mionganoni mwa watumishi wa Baraza ili kufanikisha malengo ya kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji.

Akizungumza wakati wa hotuba ya ufunguzi wa Kikao cha Mwaka cha Wafanyakazi wa EWURA CCC, kilichofanyika tarehe 22 Agosti 2024 mjini Morogoro, Mha. Ngula alieleza kuwa, ushirikiano mionganoni mwa watumishi ni silaha muhimu katika kutekeleza majukumu ya Baraza kwa ufanisi.

Aliwataka watumishi hao kutmia kikao hicho kujadili masuala ya msingi hasa katika kujadili Mpango Mkakati wa Baraza ambao ndiyo utatumika kupima kiwango cha uwajibikaji kuelekea mwisho wa mwaka wa fedha wa 2024/25.

"Nimearifiwa kwamba mtapeana majukumu kwa mujibu wa Mpango-kazi wa mwaka wa Baraza kwa mwaka wa Fedha 2024/25 na kuweka malengo kwa mujibu wa ma-

jukumu ya kazi ya kila mfanyakazi ili ziweze kupimika, jukumu hili litekelezeni kwa weledi mkubwa," alisitisiza Mha. Ngula.

Aidha, Mha. Ngula aliwapongeza wafanyakazi wa Baraza kwa juhudzi zao katika utekelezaji wa majukumu yao, na kusitisiza umuhimu wa kushirikiana ili kufanikisha malengo ya Baraza.

"Nina imani kuwa, kwa weledi na biddi yenu, EWURA CCC itaendelea kuwa nguzo muhimu katika kuhakikisha watumiaji wa huduma za nishati na maji wanahudumiwa kwa haki na ubora unaostahili na kwa mujibu wa Kanuni na Miongozo ya kiudhibiti iliyopo," alisema Mha. Ngula.

Awali Katibu Mtendaji, Bi. Stella Lupimo, akitoa neno la utangulizi, alieleza mafanikio na changamoto za mwaka wa fedha uliopita, huku akiweka msisitizo kwenye utekelezaji wa Mpango Kazi kwa mwaka wa Fedha 2024/25.

"Mwaka wa fedha uliomalizika, ulikuwa ni mwaka wa ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza licha ya changamoto ambazo nazo ziligeuzwa kuwa fursa na hivyo kusaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa," alieleza Bi. Lupimo na

kusitisiza kuwa kupitia kikao hicho mipango ya utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2024/25 itajadiliwa ili kuongeza ufanisi," alisitisiza Bi. Lupimo.

Katika Kikao hicho, Watumishi wa EWURA CCC walielimishwa kuhusu masuala mbalimbali, ikiwa ni pamodzi na Dira na Dhima Mpya ya Baraza, Mafao ya Uzeeni ambapo Afisa Matekelezo Mwandamizi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii PSSSF Bw. Philipo Kimario, aliwaelimisha watumishi hao kuhusu mifumo ya mafao inayotolewa PSSSF na namna watumishi hao wanavyonufaika moja kwa moja.

"Katika taasisi yetu, tunatoa mafao ya aina nyingi ambayo yana manufaa kwa watumishi katika nyakati tofauti. Mafao haya ni pamoda na mafao ya muda mfupi kama vile malipo ya ulemavu, kifo na ugonjwa, na pia mafao ya muda mrefu kama vile pensheni. Ni muhimu kwa watumishi kuhakikisha wanatumia vizuri mifumo hii ya mafao kwa manufaa yao, kwani ni haki zao za kisheria na zinalenga kuwasaidia katika kipindi chote cha kazi zao na hata baada ya kustaafu," alisema Kimario.

Mada zingine zilhusu masuala ya afya ya akili na maadili, utekelezaji wa sera za UKIMWI na maadili mahali pa kazi.

Katika suala la utekelezaji wa sera ya UKIMWI, Dkt. Mariam Bendera, Mratibu wa UKIMWI kutoka Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Morogoro, alisitisiza umuhimu wa watumishi kufuatilia afya zao na kuchukua hatua za kujikanga na magonjwa, hasa UKIMWI.

"Afya ni rasilimali muhimu kwa kila mtumishi. Ni lazima watumishi wafuatilie hali zao za kiafya kwa ukaribu, ikiwemo kupima afya na kuiishi kwa mfano wa kiuadilifu mahali pa kazi. Kwa kufanya hivi, wataweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi na kujiepusha na athari za kiafya amba zo zinaweza kuathiri utekelezaji wa majukumu yao." Alisema Dkt. Bendera

Kwa upande wao, watumishi kwa kauli moja walikubaliana kuweka juhudzi zaidi katika utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mwaka wa Fedha 2024/25, kuhakikisha kuwa Dira na Dhima mpya ya Baraza zinateneza kwa mafanikio na hatimaye kuongeza ufanisi wa Baraza katika kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa nishati na maji nichini.

Baraza lawafikia wafanyabiashara soko la Shilabela

Na Wadi Omari, Geita

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ya Baraza la Ushauri ka Watumiaji wa huduma za nishati na maji (EWURA CCC) Mkoa wa Geita imeendesha kampeni ya kutoa elimu kwa wananchi na wafanyabiashara wadogo katika Soko la Shilabela.

Kampeni hiyo ilianza tarehe 1 Oktoba 2024, ambapo wananchi walipata fursa ya kutembelea banda la EWURA CCC sokoni hapo na kupata mafunzo kuhusu haki, wajibu na masuala muhimu yanayohusu huduma za nishati na maji.

Katika kampeni hiyo, wananchi walifundishwa namna ya kushughulikia changamoto za huduma hizo, ikiwemo jinsi ya kuwasilisha malamakio kuhusu ankara zisizo sahihi na ucheleweshaji wa kupewa huduma.

Aidha, elimu hiyo ililenga kuwasaidia wananchi kuepuka gharama zisizo za lazima kwa kuhakikisha kuwa wana matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji, ikiwemo kutumia vifaa vya umeme na maji vyenye ubora, ili kuepuka hasara zisizotarajiwa.

Wadau hao pia walielimishwa

kuhusu moja ya sababu zinazopelekea watumiaji wa maji kupata bili kubwa ikiwemo uwepo wa mivujo kwenye miundombinu yao ya maji au matumizi holela ya maji.

Mkazi wa Mtaa wa Kumi na Nne Kambage, Bw. Joshua Zakayo, alieleza changamoto za mgao wa maji na ankara kubwa isiywendana na matumizi yake aliyoleta akipata, huku akipongeza EWURA CCC kwa elimu aliyoipata baada ya kuelimishwa kuhusu mojawapo ya sababu zinazopelekea uwepo wa ongezeko la bili za maji.

"Nawapongeza EWURA CCC kwa kutuletea elimu hii ya matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji ambapo itatusaidia kupunguza gharama zisizo za lazima, alisema Bw. Zakayo," na kuongeza kuwa, "kupitia elimu hii nitachukua hatua za kuchunguza miundombinu yangu ya maji ili kubaini ikiwa kuna mivujo inayosabisha bili kubwa." Alisema Bw. Zakayo.

Naye Bw. Yusuph John, Mfanya biashara katika soko hilo, alishukuru kwa mafunzo yanayohusu matumizi bora ya umeme kwa wafanyabiashara wanaotumia vifaa vya kielectroniki kama 'friji' na 'hita' kwa kuwapatia elimu juu ya matumizi yenyeye ufanisi

zaidi ya umeme.

"Mafunzo haya kuhusu matumizi bora ya umeme, yamekuwa ya manufaa sana kwa upande wangu kwa kuwa najihusisha na matumizi ya vifaa vya kielectroniki. Sasa nitahakikisha natumia vifaa vya kielectroniki kwa uangalifu zaidi," alisema Bw. John.

Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji Mkoa wa Gita, Bw. Dotto Paul alisema dhamira ya EWURA CCC ni kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji, na kusisiza kuwa, Kamati yake inatekeleza jukumu hilo la msingi pamoja na mambo mengine, kutoa elimu zaidi kwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa huduma hizo katika Mkoa wa Geita.

"Tuna jukumu la kuhakikisha watumiaji wanaelewa umuhimu wa kupata huduma bora za nishati na maji na hivyo tumejipanga kuwafikia watumiaji mbalimbali katika maeneo yao ya kazi na makazi na kuwaelimisha kuhusu masula muhimu ya watumiaji zikiwemo haki na wajibu wao wakati wakitumia huduma hizo," alidokeza Bw. Paul.

Kupitia programu hiyo jumla ya wadau 125 sawa na asilimia 83 ya wadau 150 waliokusudiwa kufikiwa na kuelimishwa wamefikiwa na kuifanya programu hiyo kuwa ya mafanikio.

Aidha kupitia programu hiyo jumla ya malalamiko 10 yalipokelewa, kati yake 6 yalihu huduma za maji na 4 yalihu huduma ya umeme ambapo malalamiko yote yaliwasilishwa kwa watoa huduma kwa ajili ya utatuzi.

Apunguziwa deni la maji kutoka Shilingi 1,401,055 hadi 683,795

Na Zamda Mabada, Kilimanjaro.

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kuititia Ofisi yake mkoani Kilimanjaro limemsaidia Bi. Felister Mosha, mkazi wa Shaurimoyo, Majengo Moshi kutatua changamoto ya ankara kubwa ya maji ya shilingi 1,401,055.28/= ambayo alipatiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA), ikiwa ni bili ya kuanzia mwezi Desemba, 2023 hadi Julai, 2024 ambayo kiuhalisia haikuwa ikiendana na matumizi yake.

Lalamiko hilo limetatuliwa wakati wa kikao cha usuluhishi kati ya Felister Mosha na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA) kili-choitishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na kufanyika 30/8/2024 katika Manipaa ya Moshi.

Akizungumza baada ya kikao hicho kuamuru mlalamikaji huyo kupunguziwa deni kutoka shilingi 1,401,055.28 hadi shilingi 683,795, Bi. Felister alisema hatua hiyo imefikiwa baada ya yeye kufika kwenye Ofisi za EWURA CCC mapema mwezi Julai, 2024, kwa len-

go la kutoa lalamiko lake juu ya changamoto ya kupewa deni kubwa la maji ambalo halikuwa linalingana na matumizi yake halisi na hivyo kupelekea kusitishiwa huduma.

Alieleza kuwa aliletewa bili ya mwezi Desemba ya shilingi 610,446.90/= na kusitishiwa huduma ilipofika Februari, 2024 wakati huo kiwango cha bili kikiendelea kuongezeka hadi kufikia shilingi 1,401,055.28/= mwezi Julai, 2024.

"Mara baada ya kupata changamoto hii nilienda Mamlaka ya Maji kwa ajili ya kupata maeleo kamili na kutaka kupata msaada kupunguza deni hilo, lakini walinijibu kuwa nilipe deni hilo kwani limetokana na uvujaji wa maji. Sikupewa maeleo ya kutosha, ndipo nikaelekezwa na jirani yangu kuja Ofisi ya EWURA CCC kupata msaada," alieleza Bi. Mosha. Bi. Mosha alisema "Baada ya kufika Ofisi ya EWURA CCC nilielekezwa kujaza fomu ya malalamiko ya EWURA na baada ya hapo ndipo nikaitwa kwenye kikao cha usuluhishi ambapo nilikutanishwa na watu kutoka MUWSA lengo likiwa ni kutafuta maufaka wa lalamiko langu."

Alisema, kuititia kikao hicho cha usuluhishi, ili amriwa kuwa, deni

lake lipunguzwe kutoka shilingi 1,401,055.28/= hadi kufikia shilingi 683,795/= kwa sababu ilionekana deni lilikuwa kubwa kutokana na kujumuishiwa bili ya majitaka, kulikoangalia bili ya mwisho ya mteja ambayo ndio inayolalamikiwa.

Mamlaka ilikubali kufanya marekebisho ya deni na kubakisha kiasi cha shilingi 83,795 kwani mteja alikuwa ameshalipakiasi cha shilingi 600,000/= na kurudishiwa huduma ya maji, hivyo kiasi cha shilingi 717,260.28/= kilondolewa katika deni hilo.

Bi. Mosha aliishukuru EWURA CCC kwa kumsaidia kufikisha lalamiko lake kwa Mdhibiti na hadi kupunguziwa deni lake na kuahidi kusambaza ujumbe kwa watumiaji wengine kuhusu uwepo wa Baraza mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza wakati wa kikao hicho cha usuluhishi Bi. Regina Mwanzoho, Afisa Huduma kwa Wateja MUWSA, alimuomba radhi mteja huyo kwa niaba ya Mamlaka kwa kutoshughulikia lalamiko lake kwa umakini, ukamili fu na kwa wakati.

"Tumeona udhaifu wetu wakati wa kukuhudumia mteja wetu, naamini tuna nafasi ya kurekebisha mapungufu yetu," alisema Bi. Mwanzoho.

Aliendelea kueleza kuwa, bili ya mteja wao huyo iliendelea kukua kila mwezi kwa sababu mteja wao alikuwa ameunganishwa kwenye mfumo wa majitaka na gharama zilikuwa zinakuja kwa kufuata bili ya mwisho ya maji.

Bi. Mwanzoho alisema pamoja na mteja huyo kusitishiwa huduma ya majisafi lakini huduma ya majitaka aliendelea kuitumia kwani karo na choo viliendelea kutumika, hivyo mfumo wa Mamlaka ultengeneza bili ambapo kiuhalisia ilitakiwa kuangalia bili za nyuma kabla ya ile kubwa, iliyokuwa inalamikiwa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa kikao hicho kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Nishati Na maji (EWURA) Kanda ya Kaskazini Bi. Christina Martin alitaka MUWSA kufanya marekebisco kwa kupunguza deni la majitaka na kumpatia mteja deni halisi.

EWURA CCC kuititia Kamati yake ya Watumiaji mkoani Kilimanjaro, itaendelea kutekeleza, pamoja na mambo mengine, jukumu la kutetea na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji mkoani Kilimanjaro ili kuchangia katika kuboresha huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA mkoani humo.



WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI
WA MAZINGIRA IRINGA (IRUWASA)



PIGA BURE
0800 110 122



**TUKO TAYARI KUKUHUDUMIA
SIKU SABA ZA WIKI**

0800 110 122

@iruwa.sa

@iruwasa.Iringa

"Furaha Yako Furaha Yetu"

Maswali na Majibu

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Swali: Je sheria inasema nini kuhusu muda wa ukaguzi wa mita ya maji tangu imefungwa kwa mteja ili kuhakiki kiwango cha ubora katika kupima matumizi ya mteja kwa kipindi husika?

Kwa mujibu wa Kanuni ya 51(1) ya Kanuni za usambazaji maji (The Water Supply Regulations, 2019), GN No. 828, mamlaka za maji zinapaswa kukagua na kuzihakiki mita za kupimia maji angalau mara moja ndani ya miaka 5 na kutoa taarifa ya ukaguzi.

Swali: Ni madhara yapi anayoweza kuyapata mtumiaji wa maji endapo atacheleweshaa kulipa bili yake?

Kanuni ya 51(3&4) ya Kanuni za Maji na Usafi wa Mazingira (The Water Supply and Sanitation Services (Licensing and Quality of Service) Rules, 2020, inaeleza kuwa mtoe huduma anaweza kumkatia mteja huduma ya maji endapo zitapita siku 30 tangu mteja apokee bili ya maji bila kuilipa bili husika; au kumfungulia mashtaka mahakamani endapo zitapita siku 60 bila kulipa tangu mteja apokee bili yake.

Swali: Ni nini kinachoweza kusababisha EWURA kusimamisha matumizi ya leseni kwa mtoe huduma wa umeme?

EWURA inaweza kusimamisha matumizi ya leseni kwa kipindi hadi miezi kumi na mbili ikiwa kumetokea:-

(a) Ukiukwaji wa masharti ya leseni yenye.

(b) Ukiukwaji wa masharti ya Sheria na Kanuni husika.

(c) Mwenye leseni ameshindwa kulipa tozo ya udhibiti kwa EWURA na tozo hiyo imebaki hajjalipwa kwa siku thelathini baada ya siku ambayo ilitakiwa kulipwa na Mam-laka kumpa mwenye leseni notisi kwa maandishi kuwa malipo hayo yamechelewa.

Hii ni kwa mujibu wa Kanuni 17 ya Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji na Usambazaji wa Umeme za Mwaka 2023.

Swali: EWURA CCC ni nini?

EWURA CCC ni Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Hudma za Nishati na Maji lililoanzishwa chini ya kifungu cha 30(1) cha wa Sheria ya EWURA Sura Na. 414. (EWURA Act Cap 414). Majukumu ya Baraza ni kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA ambazo ni huduma za maji, umeme, mafuta na gesi asilia.

Swali: Je nifanye nini ninapokua sijaridhishwa na huduma ninayopatiwa kutoka kwa watoa huduma za nishati na maji?

Unaweza kulalamikia huduma hiyo kwa mtoe huduma husika kwa ajili ya utatuzi wa changamoto inayokabili. Hata hivyo, unaweza pia kuwasilisha lalamiko lako kwa EWURA ikiwa mtoe huduma hatafanya kazi malalamiko yako.

Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za Utatuzi wa

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Maswali na Majibu

Malalamiko (The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Consumer Complaints Settlement Procedure) Rules, 2020, GN No. 428.

Wawenza pia kuinakiri EWURA CCC barua ya lalamiko ili kupata ushauri na usaidizi wa namna sahihi ya kuttatua changamoto inayokukabili.

Swali: Je, ni taarifa gani muhimu mamlaka za maji zinawajibika kuwapatia watumiaji wa maji?

Mamlaka za maji zina wajibu wa kuwapatia wateja wao taarifa zifuatazo:-

- Taarifa za bei za huduma na taarifa nyingine za ziada.
- Jinsi ya kusoma mita za maji na namna bili zinavyokokotolewa.
- Taarifa kuhusu mabadiliko ya bei ya huduma.
- Taarifa na kumbukumbu za rmani, mipango, na rekodi za mifumo ya usafirishaji na usamabazaji au mifumo ya ukusanyaji ili kusaidia kuwaelekeza wateja watarajiwa.
- Elimu kuhusu maudhui ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja.

Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 20(a-e) ya Kanuni za Huduma za Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira (Leseni na Ubora wa Huduma), 2020.

Swali: Je, nikiwasilisha lalamiko langu nje ya muda uliowekwa na EWURA, naweza kusikilizwa?

Ndiyo, unaweza kusikilizwa iwapo Bodi ya EWURA itaona kuwa ni haki, na ni sawa kufanya hivyo. Katika hat-

ua hii, Bodi ya EWURA itatoa Agizo la kusikizwa kwa lalamiko lako. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 30 ya Kanuni za Mamlaka ya Udhhibit wa Huduma za Nishati na Maji (Taratibu za Utatuvi wa Malalamiko ya Wateja), ya mwaka 2020 (The EWURA Consumer Complaints Settlement Rules, 2020).

Swali: Je, mteja tarajiwa wa umeme anaruhusiwa kulipia gharama za maunganisho mapya ya umeme kwa awamu, baada ya kupokea namba ya kulipia (control number)?

Ndiyo, anaweza kulipia kwa awamu. Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TANESCO, Ukurasa wa 4 kipengele cha 2, unatoa fursa hii.

Mteja anayetaka kulipia gharama kwa awamu atawasilisha maombi na kuingia mkataba na TANESCO wa kulipia gharama hizo kwa awamu.

Swali: Je, ni hatua gani za kufuata ikiwa mteja anataka kuhamisha laini ya huduma ya maji (service line)?

Mteja atafuata hatua zifuatazo ili kuhamisha laini ya huduma ndani ya eneo lake:-

Kuwasilisha maombi: Mteja anapaswa kuwasilisha ombi rasmi kwa mamlaka ya maji. Hii inaweza kufanya kwa kujaza fomu maalum au kuwasiliana na ofisi za huduma kwa wateja.

Uhakiki na Tathmini: Mamlaka ya maji itafanya uhakiki wa eneo la sasa na eneo jipya ambalo mita itahamishwa. Hii inajumuisha tathmini ya uwezo wa eneo jipya kwa

Maswali na Majibu

Maswali ya ulizwayo mara kwa mara

ajili ya kuweka mita na vilevile hali ya miundombinu ya maji.

Gharama za Uhamishaji: Mteja atalazimika kulipia gharama za uhamishaji, ambazo zinaweza kujumuisha malipo ya kazi ya ufundi, vifaa, na usakinishaji. Gharama hizi zinaweza kutofautiana kulingana na umbali wa uhamishaji, aina ya mita, na hali ya miundombinu. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 39(1) ya Kanuni za Usambazaji wa Maji na Usafi wa mazingira, (Lesseni na Ubora wa Huduma) za mwaka 2020 (The Water Supply and Sanitation Services (Licensing and Quality of Service) Rules, 2020).

Swali: Je naweza kuwasilisha maombi ya huduma za umeme pasipokufika ofisi za TANESCO?

Ndiyo, kwa sasa unaweza kuwasilisha maombi kwa kutumia aplikesheni ya nikonekt "Ni-Konekt" au kuwasilisha maombi yako kupitia tovuti ya TANESCO kupitia kiunganishi cha: <https://nikonekt.tanesco.co.tz/index.php?r=application>

Swali: Je mteja wa TANESCO ataendelea kupokea tarakimu 60 za tokeni ya umeme kila anaponunua umeme hata baada ya zoezi la maboresho ya mfumo wa mita za LUKU kukamilika?

Hapana. Mteja atapokea tarakimu/tokeni hizi mara moja pekee na baada ya hapo mita ya mteja itakuwa imeboreshwa na ataendelea kuingiza tarakimu 20

kama ilivyokuwa awali. (Hii ni kwa mujibu wa taarifa rasmi iliyotolewa na TANESCO, ambapo zoezi hili mwisho wake ulikuwa ni tarehe 24 Novemba, 2024.

Swali: Je, ni sawa kununua mitungi ya gesi ya kupikia majumbani yenye uzito pungufu, mfano mtungi wa Kg 15 unaonesha (Kg 14.0 hadi 14.9 wakati wa upimaji) ambaou unakuwa haujafika Kg 15 kamili?

Ni sawa ikiwa muuzaji amehakikisha kuwa mitungi ya gesi ina kiwango cha uzito kama inavyoelekezwa katika masharti ya Sheria ya Vipimo na Uzito (The Weights and Measures Act), kifungu cha 41(b). Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 33(1) ya Kanuni za Uendeshaji Huduma za Mafuta na Gesi (The Petroleum Liquified Petroleum Gas Operations) Rules, 2020) GN. 825.

Swali: Je, ni utaratibu gani unatumika na Mam-laka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kutoa taarifa ya katizo la maji?

Kwa mujibu wa Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa DAWASA, Kipengele cha 17(vi&vii):

- DAWASA itatoa taarifa kwa muda usiopungua masaa ishirini na nne (24) kwa tatizo la maji lililopangwa na litakaloathiri huduma kwa zaidi ya saa 4 pia DAWASA Itatoa taarifa kwa muda usiopungua masaa 12 kwa tatizo la huduma litakalodumu kwa chini ya masaa manne (4).

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Maswali na Maji

- DAWASA itawataarifu wateja wake juu ya katizo la huduma ya maji linalotokana na dharura hii ndani ya muda wa saa 2.

Swali: Nawezaje kuzuia bili kubwa ya maji?

- Kwa kufanya marekebisho ya haraka unapobaini uvujaji katika mifumo ya mabomba na kubadili vifaa vilivyo chakaa. Uvujaji mdogo kwenye bomba au choo unaweza kupoteza mamia ya lita za maji kila siku na kupelekea bili kubwa.
- Kuzingatia tabia za matumizi mazuri ya maji, kutumia maji vizuri na kwa uangalifu kunaweza kusaidia kudhibiti gharama za matumizi ya maji.

Weka utaratibu wa kufuatilia bili yako ya maji kila mwezi ili kubaini ongezeko lolote la ghafla.

Swali: Je, ni taasisi ipi inatoa leseni zinazohusu huduma za nishati na maji?

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ndiyo yenye mamlaka ya kutoa leseni zinazohusu huduma za nishati na maji. Hii ni kutokana na Kifungu cha 7(1) (b)(i) cha Sheria ya EWURA (The EWURA Act), Sura Na. 414.

Swali: Je, ni sahihi mita ya mteja wa maji kuondolewa katika eneo lake pasipo yeye kuwepo au mwakilishi wake?

Siyo sahihi mita ya maji kuondolewa katika eneo la mteja pasipo yeye kuwepo au mwakilishi wake. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 47 (1) ya

Kanuni za Maji na Usafi wa Mazingira (Ubora wa Huduma Na Leseni) za mwaka 2020 (the Water Supply and Sanitation Services (Licensing and Quality of Service) Rules, 2020); Tangazo la Serikali Na. 849).

Swali: Je, mtumiaji/mteja wa umeme anaweza kulipwa fidia ikiwa atapata hasara au madhara ya kimwili?

Ndiyo anaweza kulipwa fidia ikiwa atapata madhara ya kimwili. Hii ni kwa mujibu Kanuni ya 24(1) (2) (3) ya Kanuni za Umeme (Uzalishaji, Usafirishaji, na Usambazaji) za Mwaka 2023, Tangazo la Serikali 449, (The Electricity (Generation, Transmission and Distribution Activities) Rules, 2023, GN 449).

Kanuni hizi zinamtaka mtoe huduma kumfidia mtu yeoyote aliyepata madhara au kupoteza mali kutokana na shughuli zinazodhibitiwa ambazo zinatolewa na mtoe huduma huyo. Aidha mwathirika anapaswa kuwasilisha malalamiko yake kwa mtoe huduma kwa usuluhishi na ikitokea mwafaka umeshindikana basi malalamiko hayo yawasilishwe EWURA.

Swali: Kwa nini kuna tofauti ya gharama ya maunganisho ya umeme kwa watu wa vijijini na wa mjini ilhalii nchi ni moja?

- Ni kweli kuna tofauti ya gharama zinazozwa kwa waombaji wapya wa umeme vijijini na åawa mjini. Hii ni kwa mujibu wa Agizo la Marekebisho ya Bei za Umeme la

Maswali na Majibu

Maswali ya ulizwayo mara kwa mara

EWURA mwaka 2020, (The Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO) Tariff Adjustment (Amendment) Order, 2020) Jedwali la 1.

Maunganisho mapya kwa Kijijini ni TZS 27,000/- tu na wateja wa mjini ni kuanzia TZS 320,960 kwa njia moja ya umeme.

Swali: Je, mtumiaji akiuza maji kwa watu wengine ndani ya eneo linalopata huduma kutoka kwa mamlaka ya maji, anatenda kosa?

Ndiyo, anatenda kosa. Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ndiyo chombo kilichopewa dhama-na ya kuwafikishia huduma wateja katika maeneo ambapo mamlaka za maji zinatoa huduma.

Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 13(2) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za Usambazaji Maji za 2019 (The Water Supply and Sanitation Regulations 2019-GN 828).

Swali: Je naweza kupata tokeni ya LUKU au ankara ya maji endapo nitafuta meseji kwenye simu kwa bahati mbaya bila kwenda ofisi za Mamlaka ya maji au TANESCO?

Ndiyo. Kama una simu janja unaweza ukapata tokeni zako kwa kufuata njia zifuatazo:

- Pakua aplikesheni ya GePG Tanzania.
- Chagua huduma husika ya umeme au maji.
- Kama ni kupata tokeni uli-

zonunua nenda sehemu ya kupata tokeni ya mwisho.

- Chagua kimojawapo cha kuja-za kama vile namba ya simu uliy-onunulia LUKU, mita namba, risiti ya GePG au risiti ya benki.

- Kama unataka ankara yako ya maji chagua huduma ya maji, weka akaunti namba yako kisha utapokea.

Swali: Ni madhara gani atayapata mtumiaji wa umeme akiharibu mita au rimoti ya umeme?

Mtumiaji wa umeme atalazimika kulipia mita au rimoti aliyoiharibu. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 26 (6) (a-d) cha Sheria ya Umeme namba 10 ya Mwaka 2008 (Electricity Act, No. 10 of 2008).

Swali: Ni kwa namna gani nitapata bei za huduma za umeme zilizoidhinishwa na EWURA?

Bei za huduma zilizoidhinishwa na EWURA zitatangazwa hadharani na TANESCO kuitia magazeti, tovuti, radio, mbao za matangazo na njia nyingine rahisi kuwafikia wananchi. Hii ni kwa kwa mujibu wa Kanuni 41(1) ya Kanuni za Umeme (Usambazaji wa Huduma) za mwaka 2019 (The Electricity (Supply Services) Rules, 2019, GN. 387).

Swali: Je, ni kwa nini vituo vya mafuta vinauza mafuta kwa bei tofauti?

Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani isipokuwa bei hiso zisizidi bei kikomo (Price cap)

Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Maswali na Majibu

au kuwa chini ya bei iliyoruhusiwa (Floor Price) kama zilivyokoko-tolewa kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa tarehe 28 Januari 2022 kuitia Gazeti la Serikali Na. 57 na marekebisho ya Kanuni tajwa kuitia Gazeti la Serikali Na. 761A la tarehe 30 Oktoba 2023 na Mabadiliko ya Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja za Mwaka 2024.(The Energy and water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Products Price Setting) (Amendedment) Rules 2023-GN. 716A).


Swali: Je ni fundi umeme mwenye vigezo vipi atumike kufunga mifumo ya umeme ndani ya nyumba?

Fundi mwenye leseni kutoka

EWURA ndiyo ana sifa za kufunga mifumo ya umeme ndani ya nyumba. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 19(1&2) ya Kanuni za Huduma za Ufungaji wa Umeme, The Electricity (Electrical Installation Services) Rules, 2022.

Swali: Je, ni nani anayewajibika kuilinda dira (mita) ya maji aliyofungiwa mteja?

Mto huduma anawajibika kutunza usalama wa dira ya maji aliyofungiwa mteja. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 39 (1) (e) ya Kanuni za Maji na Usafi wa Mazingira (Ubora wa Huduma na Leseni) ya mwaka 2020 (The Water Supply and Sanitation Services (Licensing and Quality of Service) Rules, 2020, GN. No. 849).





Nukuu Maridhawa

“

Nimefurahi kuwaona EWURA CCC katika tamasha hili, na ninawapongeza kwa kazi kubwa mnayofanya ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu faida za katumia nishati safi ya kupikia. Hii ni hatua kubwa na muhimu kwa taifa katika kuhakikisha wananchi wanapata uelewa wa matumizi sahihi ya nishati hii, ambayo ni salama na rafiki kwa mazingira.

-- *Naibu Waziri wa Nishati,
Mhe. Judith Kapinga*

”

Nina imani kuwa, kwa weledi na bidii yenu, EWURA CCC itaendelea kuwa nguzo muhimu katika kuhakikisha watumiaji wa huduma za nishati na maji wanahudumiwa kwa haki na ubora unaostahili na kwa mujibu wa Kanuni na Miongozo ya kiudhibiti iliyopo.

-- *Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC),
Mhandisi David Ngula*